SportPesa
TZS. 667,771,400
NI YA KWAKO WIKI HII, BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Utafiti** wabaini ugonjwa unaopunguza uwezo wa kufikiri

UKURASA 4

Nipashe
Jumatano Novemba 10, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580760
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



**De Jong kubadilishwa na Sterling**

UKURASA 23

# Wabunge wang'aka kilimo kutothaminiwa

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 4
**WANAFUNZI WAFA KWA KUFUKIWA NA KIFUSI**
WANAFUNZI watatu, wakiwamo wawili wa familia moja, wamefariki dunia baada ya kufukiwa na kifusi...

UKURASA WA 5
**MAREKANI YATOA MABILIONI KWA HOSPITALI YA BUGANDO**
UBALOZI wa Marekani nchini umetoa msaada kwa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Ziwa ya Bugando ambao...

UKURASA WA 8
**MATUMIZI GESI ASILIA YALIVYOOKOA TRIL. 38/-**
KATIKA kipindi cha mwaka 2004 hadi Juni 2020, matumizi ya gesi asilia ya Mnazi Bay na Songo Songo yamesaidia..



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa, Freeman Mbowe (katikati) na wenzake, wakiwa chini ya ulinzi wa askari magereza, baada ya kuwasili katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, Sinza mkoani Dar es Salaam jana, kusikiliza kesi inayomkabili. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Korti yatupa pingamizi la kielelezo kesi ya Mbowe

UKURASA 2



Pundamilia anayeishi na wafugaji katika eneo la pori la Kijiji cha Nampungu Kumwembe, wilayani Tunduru, mkoani Ruvuma, akiwa pamoja na punda wa kufugwa jana. **PICHA: STEVIE CHINDIYE**

## Pundamilia aishi na wafugaji, waiomba serikali imchukue

UKURASA 3

**MICHEZO** FRANCO ATOA SABABU KUKUBALI KUTUA SIMBA UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

KESI YA MBOWE

# Korti yatupa pingamizi kutopokewa kielelezo

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi imeamua kutupilia mbali pingamizi la mawakili wa utetezi la kutaka hati ya kukamatia mali kama kielelezo kisipokelewe mahakamani kwa sababu kuna makosa ya sheria.

Jaji Joachim Tiganga, alisema mawakili wa utetezi hawakuonyesha athari wanayoweza kupata kwa kukosewa kwa kifungu hicho, makosa yaliyopo yanarekebishika na kuamua kutupilia mbali pingamizi la kutaka kielelezo kisipokelewe.

Hata hivyo, mahakama hiyo ilikubali hoja za mawakili wa utetezi kwamba kifungu cha sheria kilichotumika kwenye hati ya kukamatia mali namba 38(3) kilikosewa hakijawahi kufanyiwa marekebisho mwaka 2018.

Uamuzi huo ulitolewa jana katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na wenzake watatu baada ya Wakili Peter Kibatala na jopo lake kupinga hati ya ukamataji kupokelewa mahakamani kama kielelezo kwa sababu kuna makosa ya sheria.

Akisoma uamuzi, Jaji Tiganga alisema mawakili wa utetezi kwa ujumla wao walidai katika fomu ya kukamata mali iliyotolewa na shahidi wa nane wa Jamhuri, Mrakibu wa Polisi Jumanne Malangahe imenukuliwa kifungu cha sheria namba 38(3) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai sura ya 20 kilichofanyiwa marekebisho mwaka 2018.

Upande huo ulidai hakuna marekebisho yaliyofanyika mwaka huo, yalifanyika mwaka 2013 na sheria iliyopo ilifanyiwa mapitio mwaka 2019.

Upande wa mashtaka ulikiri kwamba hakuna marekebisho yaliyofanyika kwa sheria hiyo mwaka 2018, lakini waliomba mahakama ione kwamba nyaraka imekidhi vigezo ipokelewe kama kielelezo.

Jaji Tiganga alisema baada ya kupitia hoja zote pingamizi liko wazi na moja kwa moja, ni kwamba kifungu namba 38(3) hakikuwahi kufanyiwa marekebisho mwaka 2018, mara ya mwisho kilirekebishwa mwaka 2013.



"Kifungu hicho cha sheria kimenukuliwa kimakosa, lengo la kunukuu sheria ni kuipa mahakama mamlaka ya kusikiliza shauri, nyaraka iliyopo si ya kuleta maombi ya kutoa amri fulani.

"Nakubaliana na hoja ya upande wa Jamhuri kwamba baada ya mabadiliko, sheria iliitaka mahakama ikifanyie uamuzi iangalie haki zaidi.

"Kanuni inasema lalamiko la sheria kunukuliwa kimakosa haitoshi kuifanya mahakama kusema nyaraka hiyo ina makosa itupwe.

"Anayeomba itupwe lazima aseme athari anayopata kwa kupokelewa kielelezo hicho chenye kifungu cha sheria chenye makosa.

"Jambo lililoelezwa marekebisho ya mwaka 2018 haijaelezwa athari wanayopata kwa kukosewa, mahakama inaona mapungufu yanarekebishika, nyaraka inapokelewa kama kielelezo, pingamizi linatupiliwa mbali," alisema Jaji Tiganga.

Kielelezo hicho kilikuwa hati ya kukamata bastola aina ya Luger namba A5340, risasi tatu, simu na line mbili, vyote inadaiwa alikutwa navyo Adamu Kasekwa.

SP Jumanne akiendelea kutoa ushahidi alidai baada ya kuwakamata washtakiwa Kasekwa na Mohammed Ling'wenya Agosti 5, mwaka 2020, waliwapeleka Kituo cha Polisi Moshi na Agosti 6, mwaka huo waliondoka Moshi kuwapeleka washtakiwa Dar es Salaam na walifika Agosti 7, mwaka 2020 alfajiri.

Alidai alipewa jukumu la kumuhoji Ling'wenya na alimuhoji kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa tano asubuhi, alimpa haki zake zote, alikubali kuhojiwa akiwa peke yake na katika mahojiano alikiri kuhusika na tuhuma za kula njama kufanya vitendo vya kigaidi.

Shahidi alidai alipigiwa simu Julai 21, mwaka 2021 na Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Kamishna wa Polisi Camilius Wambura akimtaka afike Dar es Salaam.

Anadai Julai 22, 2021 alifika Dar es Salaam Kituo cha Polisi cha Kati akitakiwa kumuhoji Mbowe.

"Saa 6.50 usiku Mbowe aliletwa kwangu na Inspekta Chota, nilimpa haki zake zote, nilimwambia anatuhumiwa kwa kula njama kufanya ugaidi, nilimuuliza anataka kuhojiwa mbele ya nani, alijibu anataka mbele ya Mwanasheria wake Fredrick Kihwelo.

"Kwa siku hiyo mwanasheria hakuweza kupatikana hadi kesho yake saa saba mchana, nilijitambulisha na kumfahamisha tena haki zake, nikamwambia tuendelee na mahojiano, Mbowe alijibu hayuko tayari kutoa maelezo yake mbele ya Ofisa wa Polisi, Mwanasheria alisaini, mtuhumiwa alisaini na mimi niliweka saini yangu," alidai SP Jumanne.

SP Jumanne kwa kuongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Robert Kidando walitaka kutoa maelezo hayo ya Mbowe kama kielelezo, lakini Wakili wa Utetezi, Nashon Nkungu alipinga na kabla hajaendelea kuwasilisha hoja, Jaji alihoji kama maelezo hayo yanabishaniwa katika kesi hiyo.

Jaji Tiganga alisema kinachobishaniwa ndicho kinachotolewa kielelezo. Wakili Kidando aliomba muda wakatafakari kisha wajibu hoja hiyo.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Halfani Bwire, Kasekwa na Ling'wenya ambao wanakabiliwa na mashtaka sita ikiwamo kula njama na kufanya vitendo vya ugaidi.

**MAHAKAMA YAINGIA KWENYE KESI NDOGO NDANI YA KUBWA**

Mahakama imelazimika kwa mara ya pili kuingia kwenye kesi ndogo ndani ya kesi kubwa baada ya mawakili wa utetezi kupinga kupokelewa kwa maelezo ya Ling'wenya kwa madai hakuwahi kufikishwa Kituo Kikuu cha Polisi Dar es Salaam na akichukuliwa kwa maelezo kwa vitisho.

Mahakama hiyo ilishawahi kuingia kwenye kesi ndogo wakati upande wa utetezi wanapinga kupokelewa kwa maelezo ya mshtakiwa Kasekwa na kila upande ulikuwa na mashahidi watatu.

Kabla ya kuwasilisha pingamizi upande wa Jamhuri uliamua kuondoa nia ya kuwasilisha maelezo ya onyo ya Mbowe kama kielelezo mahakamani.

Baada ya hapo shahidi alitakiwa kuendelea na ushahidi wake na kudai anaweza kutambua maelezo ya onyo ya Ling'wenya hapo mahakamani.

Baada ya kuyatambua shahidi aliomba kuwasilisha maelezo hayo kama kielelezo katika kesi hiyo, lakini upande wa utetezi kupitia Wakili Kihwelo alipinga kupokelewa kwa maelezo hayo.

Alisimamia msingi kuwa mshtakiwa huyo hajawahi kupelekwa kafika Kituo Cha Polisi Kati katika tarehe tajwa wakati wa kurekodi maelezo Agost 7, 2020 kama alivyodai shahidi.

Mshtakiwa huyo anadaiwa kuteswa wakati wa kutia saini yake katika maelezo ambayo hajawahi kuandika kwa maelezo yake katika Kituo cha Polisi Mbweni na hakuruhusiwa kusoma maelezo hayo.

Mahakama iliahirishwa hadi leo, mashahidi kwenye kesi ndogo wataanza kusikilizwa.

# Wabunge wang'aka kilimo kutothaminiwa

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WAKATI serikali ikiwasilisha bungeni mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2022/23, wabunge wameng'aka mpango huo kutoeleza mikakati ya kuinusuru sekta ya kilimo.

Wamesema hivi sasa kuna malalamiko mengi katika sekta hiyo ikiwamo wakulima kulia bei ghali ya mbolea, kutokupata mbegu, uhaba wa maofisa ugani, lakini mpango huo haujaeleza namna ya kutatua matatizo hayo.

Mbunge wa Kongwa na Spika wa Bunge, Job Ndugai, alisema jana kuwa eneo la kilimo ndilo lililochangiwa kwa kiwango kikubwa na wabunge katika mjadala huo kwa sababu mpango haujaainisha mikakati iliyowekwa kukinusuru kilimo hususani suala la mbolea na pembejeo.

Wakichangia mpango huo, Mbunge wa Mbeya Vijijini, Manase Njeza, alisema nchi mbalimbali duniani ikiwamo Zambia, zimekipa kipaumbele kilimo hususani kilimo cha mahindi katika kuinua uchumi wao.

"Sisi katika mpango wote hatujaweka kilimo kwenye ushindani wala kueleza tuna mkakati gani, tunataka kilimo kiwe namba moja ili Watanzania zaidi ya milioni 20 waweze kunufaika," alisema Njeza.

Mbunge wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu, alisema endapo serikali inahitaji kuwekeza kwenye sekta ya kilimo, lazima mpango huo ueleze kwamba zinahitajika angalau Sh. trilioni moja.

Alisema fedha hizo zitasaidia kupatikana kwa maofisa ugani wa kutosha na mbolea, vinginevyo kilimo hakiwezi kuwa chenye tija kwa wakulima.

Alibainisha kwenye eneo la uwekezaji wa mabwawa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji serikali katika mpango huo haijasema mikakati yake kuwasaidia wakulima nchini.

"Leo ukienda kila halmashauri inaongelea upungufu wa maofisa ugani ambao ni wataalamu, leo wakulima wengi wanalima kilimo cha kurithi, kilimo cha mazoea ambacho mtu anapata debe mbili au tatu kwenye heka moja, kitu ambacho anapoteza muda. Eneo hili lilipaswa mpango ueleze bayana namna gani tunaweza kumsaidia mkulima kule kijijini aweze kutajirika kupitia kilimo," alisema Mtaturu.

Mbunge wa Viti Maalum, Stella Fiyao, alisema sekta ya kilimo ni muhimu kwa kuwa inachangia asilimia 26 ya ukuaji uchumi wa nchi, hivyo inatakiwa kupewa kipaumbele na kuitaka serikali itumie njia ya dharura kutatua changamoto ya pembejeo.

"Awali mbolea ilikuwa inauzwa Sh. 65,000 kwa mfuko wa kilo 50, lakini sasa hivi inauzwa Sh.120,000 jambo ambalo hakuna mkulima anayemudu, hivyo serikali inapaswa kulichukulia jambo hili kwa dharura maana hali ni mbaya kwenye maeneo mengi," alisema Fiyao.

Mbunge wa Viti Maalum, Subira Mgalu, aliishauri serikali kuangalia kikwazo cha kupanda kwa bei ya mbolea, fedha zitengwe kwa ajili ya kuhakikisha inapatikana kwa bei nafuu.

Mbunge wa Muleba Kusini, Charles Mwijage, aliishauri serikali kujenga kwa haraka kiwanda cha mbolea, ili bidhaa hiyo ipatikane badala ya kusubiri.

Mbunge wa Hanang', Samweli Hayuma, alisema bila kuwekeza kwenye kilimo, taifa halitaweza kupiga hatua kwa sababu sekta hiyo inaajiri idadi kubwa ya Watanzania.

Alisema hivyo serikali inapaswa kuwekeza fedha za kutosha kwenye kilimo na wataalamu wake ili kiwe na tija kwa taifa.

Mbunge wa Viti Maalum, Dk. Christine Ishengoma, alisema kilimo ni sekta inayopaswa kupewa kipaumbele namba moja kutokana na umuhimu wake kwenye mpango wa maendeleo, lakini mpango huo haijadadavua.

Alisema bajeti ya kilimo inapaswa iongezeke kutoka Sh. bilioni 250 mwaka 2021/22 hadi Sh. bilioni 500 mwaka 2022/23 kwa kuangalia mpango.

Mbunge wa Mbinga Mjini, Jonas Mbunda, alisema: "Sijaona sehemu yoyote ambayo wakulima wametajwa watasaidiwa kuhusu pembejeo. Mpango haujaonyesha muunganiko kuanzia uzalishaji, masoko hadi viwanda. Mpango ulipaswa kueleza mikakati ya upatikanaji wa mbolea kwa wakulima."

Mbunge wa Singida Magharibi, Elibariki Kingu, alisema kama kweli serikali imedhamiria kumkomboa mkulima, mpango huo ulipaswa kueleza utatuzi wa suala la kupanda kwa bei ya mbolea.

Mbunge wa Kuteuliwa, Riziki Lulida, alisema: "Bado tuna changamoto katika sekta ya kilimo, tunahitaji nguvu ya ziada kwenye kilimo. Tumepata fedha za msaada za corona lakini kwenye mgawanyo hakuna hata senti moja iliyoelekezwa kwenye kilimo.

"Tufanye mchakato wa kuingiza fedha hizo kwenye kilimo. Mpango wa Maendeleo ulipaswa kutaja mkakati wa kumwinua mkulima," alisema mbunge huyo.

TANGAZO

# Pundamilia aishi mwaka mmoja na wafugaji, waomba serikali imchukue

**Na Stevie Chindiye, TUNDURU**

SERIKALI imeombwa kumchukua pundamilia anayeishi kambi ya wafugaji kwa mwaka mmoja sasa ili kuipunguzia familia hiyo tatizo la kugombana na wananchi wanaomtafuta mnyama huyo kwa ajili ya kitoweo.

Ombi hilo lilitolewa na wafugaji wa jamii ya Kisukuma wanaoishi na pundamilia huyo, walidai kitendo cha viongozi kukaa kimya na kuwaacha waendelee kuishi na mnyama hiyo kimewaweka kwenye matatizo na hofu kutokana na kuwapo kwa tishio kutoka kwa baadhi ya watu kumnyemelea ili wamfanye kitoweo.

Wakifafanua taarifa hiyo kwa nyakati tofauti, wanafamilia hao Emmanuel Matonange, Miru Matonange na Mawele Matonange, walisema pundamilia huyo alionekana akiwa amefuatana na punda wa kufugwa Desemba 2020.

Walisema siku zilizofuata waliondoka na mnyama huyo akiwa amefuata na kundi la punda wa kufugwa na ng'ombe na kwenda kumuacha kwenye pori, lakini kilicho washangaza kila walipofanya hivyo pundamilia huyo alifuata nyayo na kurudi kambini kwao.

Walisema baada ya jaribio hilo kushindikana walitoa taarifa kwa uongozi wa Serikali ya Kijiji cha Nampungu ili kuepuka mkono wa sheria wa kuwa na nyara ya serikali bila kibali.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Nampungu, Mohammde Bwanali, alikiri kuwapo taarifa ya mnyama huyo katika kambi ya wafugaji na alipiga simu kwa ofisa wanyamapori wa wilaya hiyo na kumjulisha juu ya uwapo wa mnyama huyo.

Pia maofisa kutoka Hifadhi ya Taifa ya Nyerere (TANAPA), walipigiwa simu kutaarifiwa hali iliyomfanya ajiridhishe kuwa sasa mnyama huyo angeondolewa katika maeneo hayo, lakini cha kushangaza waliwachukua na kuwapeleka polisi wafugaji hao na kumuacha mnyama huyo mikononi mwao.

Kaimu Ofisa Ardhi na Maliasili Wilaya ya Tunduru, Ombeni Simon Hingi, alisema tayari suala hilo wameliwasilisha ofisi ya Waziri wa Maliasili na Utalii kwa ajili ya hatua za utekelezaji.

"Hatujajua ni kwanini mnyama huyo aliingia katika kundi hilo na kuanza kuishi kirafiki na wanyama wanaofugwa, hivyo ili kujua chanzo chake inafaa watafiti kutoa Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI) kwenda katika maeneo hayo na kufanya utafiti ili kujiridhisha na sababu ya tukio hilo," alisisitiza Hingi.

Ofisa Wanyamapori wa Wilaya ya Tunduru, Limbega Hassan, alisema kuwa taarifa zinaonyesha kuwa pundamilia hao walikuwa wawili, mmoja aliuawa na wananchi wa eneo hilo na wanahisiwa kutoka kwenye hifadhi ya jamii ya Chingoli au waliachwa na wenzao katika eneo la mapito ya ushoroba wa hifadhi za selous kwa upande wa Tanzania na Niasa kwa upande wa nchi jirani ya Msumbiji.

Alisema kwa sasa wanaendelea kufuatia nyendo za mnyama huyo kwa njia za kiintelijensia wakiwa wanashirikiana na uongozi wa serikali ya kijiji hicho hadi zoezi la kumwondoa mnyama huyo litakapokamilika.



Pundamilia anayeishi na wafugaji katika eneo la pori la Kijiji cha Nampungu Kumwembe, wilayani Tunduru. **PICHA: STEVIE CHINDIYE**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

## TANGAZO KWA UMMA

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, ipo katika hatua ya maandalizi ya mradi wa Uendelezaji wa Bonde la Mto Msimbazi (Msimbazi Basin Development Project) kwa kutumia fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia. Mradi huu utatekelezwa na Wakala wa Barabara za Mijiji na Vijijini (TARURA) kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Halmashauri ya Manispaa za Kinondoni, Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo na Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe na Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS) kwa niaba ya Wizara husika zilizotajwa hapo juu.

**Mradi unatarajiwa kutekeleza masuala yafuatayo.**

1. Kukabiliana na kujikinga na mafuriko; Mradi unatarajiwa kujenga miundombinu ambayo itakuwa na uwezo mkubwa wa kupeleka maji baharini bila kutuama au kufurika katika maeneo ya bondeni. Miundombinu hiyo itajumuisha kuimarisha kingo za mto katika maeneo korofi ili kudhibiti mmomoyoka wa udongo kwa maeneo ya kati na mwanzo wa mto Msimbazi; kujenga makinga mchanga (sand traps) katika maeneo ya kimkakati; kujenga vituo/karakana za kutunza mto; kuhamisha wahanga wa mafuriko katika maeneo ya mabondeni; kuchimba na kupanua mto kuanzia barabara ya Kawawa hadi Daraja la Selander; na kujenga matuta yenye vimo tofauti kwa ajili ya kuruhusu maji kupita kwa usalama katika kipindi cha mafuriko; kuruhusu matumizi mbalimbali ya ardhi ikiwemo city park na uendelezaji wa maeneo ya makazi na biashara.

2. Ujenzi wa Miundombinu Stamihilivu ya Usafiri; Mradi unatarajiwa kujenga daraja jipya la Jangwani ambalo litakuwa na kimo kirefu ambacho hakitaathiriwa na mafuriko. Vilevile mradi utaboresha miundombinu ya usafiri (yaani barabara na madaraja) yaliyoungana na Bonde la Mto Msimbazi ambayo yanaathiriwa na mafuriko.

3. Udhibiti wa Mmomonyoko wa Udongo na Usimamizi wa Taka Ngumu; Mradi unatarajiwa kufanya kazi mbalimbali ambazo zitazuia mmomonyoko wa udongo na kudhibiti taka ngumu ili maji ya mvua yaweze kupita bila kizuizi kuelekea baharini. Kazi hizo zitahusisha upandaji miti katika misitu ya Pugu na kingo za mto, utunzaji wa mikoko na maeneo oevu, kuendesha programu ya usimamizi wa taka ngumu katika Kata zote zilizopo katika bonde la mto Msimbazi.

4. Usimamizi wa Mipango Miji katika "Msimbazi Special Planning Area"; Matuta yatakayojengwa na mradi yatapelekea kuwepo na maeneo salama kwa ajili ya "City Park" na uendelezaji wa mji (makazi na biashara) pembezoni mwa bonde la mto Msimbazi kama ilivyopendekezwa katika Mpango wa Fursa wa Msimbazi (Msimbazi Opportunity Plan). Mradi utasaidia kuandaa mpango wa kina wa matumizi ya ardhi (Detailed Land Use Plan) ambao utakuwa shirikishi kwa wadau wote. Vilevile mradi utazijengea uwezo mamlaka husika ili ziweze kusimamia utunzaji wa "City Park" na uendelezaji wa mji kadiri ya matumizi ya ardhi yaliyopangwa.

Lengo la tangazo hili ni kuujulisha umma na wadau wa Bonde la Mto Msimbazi kuwa timu za wataalam kutoka Taasisi husika pamoja na Wataalam Washauri zinazofanya upembuzi yakinifu na usanifu zitapita katika baadhi ya maeneo ili kufanya mashauriano na wadau kwa njia mbalimbali ikiwemo mikutano, mahojiano na dodoso. Tarehe, muda na mahali pa kufanya mashauriano zitatolewa kwa wakati muafaka. Aidha, tahadhari zote kuhusiana na UVIKO -19 zitachukuliwa katika kipindi hiko.

**KATIBU MKUU**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa:**
**Baruapepe: cities.project@tamisemi.go.tz; cities.project@yahoo.com**
**Simu: +255 22 270 0769**

2165602



Mkurugenzi wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB), Dk. Anselm Mushi (aliyevaa tai), akipata maelezo kutoka kwa mtaalamu wa teknolojia kutoka Kampuni ya Twiga Foods Ltd, jijini Nairobi, nchini Kenya juzi, alipotembelea kuona na kujiridhisha uwezo wa kampuni hiyo kusambaza nafaka kabla ya kuingia mkataba wa uuzaji mazao ya bodi hivi karibuni. Kushoto ni Mtendaji Mkuu wa Kampuni hiyo, Yebeltal Getachew. **PICHA: WIZARA YA KILIMO**

# Utafiti wabaini ugonjwa unaopunguza kasi kufikiri

**Na Christina Mwakangale**

WAGONJWA 524, sawa na asilimia 43.6 ya wagonjwa wa nje 1,201 wanaougua shinikizo la juu, wana mabadiliko hasi ya ubongo na kuathiri uwezo wa kufikiri, kutunza kumbukumbu na ustahimilivu wa mambo kupungua, hususan ambao hawaudhibiti ugonjwa huo.

Hayo yamebainika katika utafiti mpya nchini uliotolewa juzi na Taasisi ya Jakaya Kikwete (JKCI), uliohusisha wagonjwa hao ambao wastani wa umri wao ulikuwa miaka 58, wanawake wakiwa theluthi mbili ya waliofanyiwa uchunguzi na kuhudhuria kliniki katika taasisi hiyo.

Kwa mujibu wa Mtafiti Mkuu, Daktari Bingwa na Mratibu wa Utafiti kutoka JKCI, Dk. Pedro Pallangyo, utafiti ulianza kufanyika Machi mwaka jana na kukamilika Februari mwaka huu, ukihusisha wagonjwa 1,201 ambao wote wanaugua shinikizo la juu la damu waliopo kwenye tiba na kuhudhuria kliniki.

Bingwa huyo pia kwenye magonjwa ya moyo, alisema utafiti huo ulilenga kuangalia mabadiliko ya kwenye mfumo wa fahamu, ubongo na madhara yatokanayo na shinikizo la damu la muda mrefu. Akifafanua zaidi, Dk. Pedro alisema kwamba shinikizo la damu ni ugonjwa unaoongoza duniani kote katika magonjwa ya moyo, pia ni kati ya magonjwa yanayoongoza kuathiri zaidi watu kuliko maradhi mengine.

"Shinikizo la juu limekuwa kwa muda mrefu, linahusisha matokeo hasi kwenye ubongo wa mwanadamu na kuathiri mishipa ya damu kwenda kwenye ubongo. Wagonjwa wa shinikizo la damu muda mrefu uwezo wa ubongo wao unapungua, zaidi hasa ambao hawadhibiti shinikizo la damu," alisema Dk. Pedro.

"Wasiodhibiti shinikizo la damu kwa kiwango cha kitaalamu yaani 140 kwa 90 ndio hasa wanaathiri zaidi uwezo wa ubongo wao," alifafanua.

Alibainisha kwamba shinikizo la juu linasababisha uwezo kifikra kuwa mdogo, pia humpunguzia binadamu kuwa na kauli za kustahimilivu au kistaarabu, pia wagonjwa hao kumbukumbu zao hupotea.

Mtafiti huyo anafafanua kwamba, utafiti huo wa kwanza kufanyika nchini na kuwahusisha mabingwa wa moyo kutoka taasisi hiyo, umelenga kubaini kilichoko kwenye jamii hususan mabadiliko kwenye ubongo na namna wagonjwa wanavyoishi na tatizo hilo.

"Zaidi ya robo tatu ya washiriki wote wa utafiti huu, walikuwa na uzito mkubwa, asilimia 17 walikuwa na kisukari, asilimia nane wana historia ya kupata kiharusi na asilimia sita uwezo wa mioyo yao ulikuwa umepungua.

"Asilimia 17 walikuwa na matatizo ya figo ya kudumu, asilimia 54 wana upungufu wa damu na karibu theluthi moja ya wagonjwa wote walikuwa na lehemu 'cholestrol' kwenye damu," alisema Dk. Pedro.

Bingwa huyo alisema mabadiliko ya ubongo yaliyobainika katika utafiti huo yalionyesha wagonjwa 524, sawa na asilimia 43.6, walikutwa na mabadiliko hasi kwenye ubongo.

Dk. Pedro alisema tatizo la upungufu wa uwezo wa ubongo wa wagonjwa hao, waliokuwa na elimu ya kiwango cha shule ya msingi au wasio na elimu kabisa, walikuwa na uwezekano mara tatu zaidi kuwa na mabadiliko hasi kulinganishwa na walio na elimu ya sekondari na kuendelea.

Alisema wahusika waliokuwa hawana kazi au kustaafu walikuwa na ongezeko la asilimia 70 la mabadiliko hasi ya ubongo kulinganishwa na walio na shughuli za kila siku za kujipatia kipato.

"Watu wanaishi mazingira ya kijijini katika utafiti huu, kwa asilimia 80 walikuwa na ongezeko la kuwa na upungufu wa uwezo wa ubongo kuliko waliopo mijini," alisema bingwa huyo.

Mtaalamu huyo aliendelea kubainisha kuwa wagonjwa walio na ugonjwa wa figo wa kudumu kwa asilimia 70 walibainika kuwa na mabadiliko hasi ya utendaji kazi na uwezo wa ubongo kulinganishwa na ambao figo zao bado zipo kwenye hali nzuri.

"Utafiti umeonyesha asilimia kubwa ya ripoti zilizoripotiwa kwenye jamii iliyokuwa na kiwango kikubwa na shinikizo la damu, walionekana wana mabadiliko hasi kwa kiwango kikubwa kuliko wale ambao hawaugui ugonjwa huu.

"Tukashauri nusu ya wagonjwa wote tuliowahoji ambao ndio wameathirika zaidi na mabadiliko ya ubongo, watoa huduma watoe elimu ili wajifunze kudhibiti shinikizo la damu lisilete madhara zaidi kwenye ubongo.

"Madaktari katika matibabu yao wafanye utafiti zaidi kuhusu mabadiliko hasi kuwasaidia wanaoishi na ugonjwa huu," alisema Dk. Pedro.

## WANAOUGUA SHINIKIZO

Bingwa wa Magonjwa ya Moyo kutoka JKCI, Dk. Tatizo Waane, alisema kuna ongezeko la wagonjwa wanaougua shinikizo la juu la damu, figo na kisukari.

Alisema mtindo wa maisha sababu ya ongezeko hilo, akiwataka Watanzania wabadili mtindo wa maisha kwa kufuata mlo wenye lishe bora, kuepukana na magonjwa yasiyoambukiza ambayo huua zaidi, hasa shinikizo la juu la damu.

Alibainisha kuwa kati ya Watanzania wanaofahamu kuwa wana shinikizo na kutumia dawa ni asilimia 30, huku asilimia 70 wakiwa hawajui na hawatumii dawa na kuwa katika hatari ya matatizo ya moyo.

Dk. Waane aliyasema hayo alipowasilisha mada kwa wanahabari Desemba mwaka jana kuhusu uhusiano wa magonjwa yasiyoambukiza na yanayoambukiza katika warsha iliyoandaliwa na Chama cha Magonjwa Yasiyoambukiza Tanzania (TANCDA).

# Wanafunzi wafa kwa kufukiwa na kifusi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WANAFUNZI watatu, wakiwamo wawili wa familia moja, wamefariki dunia baada ya kufukiwa na kifusi cha mchanga katika machimbo ya Kiembeni, Kata ya Msangani Wilaya ya Kibaha.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alithibitisha jana kutokea kwa tukio hilo. Alisema miili ya watoto hao ilipatikana Novemba 5, mwaka huu, majira ya saa 2:00 asubuhi katika kitongoji cha Kiembeni.

Alisema watoto hao walipotea Novemba 4 na familia kwa kushirikiana na Polisi walifanya msako ambao miili ya watoto hao ilipatikana katika machimbo hayo.

Kamanda Wankyo aliwataja wanafunzi hao kuwa ni Omari Ramadhani (14) mwanafunzi wa darasa la tano, Hamis Ramadhani (11) wa darasa la nne, wote wanafunzi wa Shule ya Msingi Kibaha na Muhsin Killian (11) wa darasa la nne katika Shule ya Msingi Msangani.

Mmoja wa wazazi wa Muhsin, alisema kabla ya kupotea, watoto hao waliondoka nyumbani wakidai wanaenda kucheza maeneo ya karibu lakini hawakurejea hadi walipopatikana wakiwa tayari wamefariki dunia.

Wankyo alisema taarifa za awali zimeeleza kuwa watoto hao walikuwa na tabia ya kutembelea na kufanya michezo katika machimbo hayo ya mchanga.

Wakati huo huo, Kamanda Wankyo alisema Jeshi la Polisi limepokea taarifa za kupotea kwa Charles Mtweve (67) mkazi wa Kijiji cha Mafizi Kata ya Gwata Wilaya ya Kisarawe ambaye anadaiwa alitoweka nyumbani kwake Novemba 4 akiwa na rafiki zake wawili.

Kwa mujibu wa Kamanda Wankyo, Mtweve na wenzake walitoka nyumbani wakiwa wanakwenda katika pori la kijiji cha Sungura kilichoko Ngerengere Wilaya ya Morogoro kwa ajili ya kwenda kuwinda.

Alisema Meshak Msemi (50) mkazi wa Kijiji cha Mafizi na Juma Athumani (40) wa Kijiji cha Gwata waliokuwa wameongozana na Mtweve, inadaiwa baada ya kuua wanyama wawili aina ya nguruwe pori, walirejea nyumbani lakini Mtweve hajafika nyumbani hadi sasa na haijulikani aliko.

Kutokana na kutoonekana mpaka jana, Wankyo alisema wanashirikiana na vyombo vingine kufuatilia aliko Mtweve.

# Marekani yatoa mabilioni kuboresha huduma Bugando

**Richard Makore na Neema Emmanuel,**
MWANZA

UBALOZI wa Marekani nchini umetoa msaada kwa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Ziwa ya Bugando ambao umesaidia kuboresha maabara ya kisasa ambayo itakuwa na uwezo wa kupima virusi vya corona badala ya kutumia vipimo hivyo kwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Msaada huo wenye thamani ya Sh. bilioni 36 mbali na kuboresha maabara ya kisasa ya Bugando, pia umetumika kugharamia matibabu kwa wenye virusi vya Ukimwi pamoja na maeneo mengine muhimu katika utoaji wa huduma za afya.

Akizungumza katika ziara ya Balozi wa Marekani katika hospitali hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Bugando, Dk. Fabian Massaga, alisema maabara hiyo licha ya kupima UVIKO - 19, pia itapima magonjwa ya saratani, homa ya ini, kifua kikuu, virusi vya Ukimwi na vinasaba.

Dk. Massaga alisema maabara hiyo inavyo vifaa vyote vya kisasa pamoja na wataalamu na kwamba kwa Kanda ya Ziwa, uchunguzi wa magonjwa mengi utafanyika hospitalini hapo.

Aliishukuru serikali ya Marekani kupitia ubalozi wake nchini kwa kuendelea kuisaidia Bugando na wananchi wa Kanda ya Ziwa.

"Siku hii tumeweka historia katika hospitali hii. Ubalozi wa Marekani umetoa msaada mkubwa sana katika hospitali hii. Eneo walilotusaidia ni pamoja na kupambana na Ukimwi ndani ya hospitali kwa kuwa wametoa msaada mkubwa katika kutengeneza maabara ambayo inafanya kipimo vyote muhimu," alisema Dk. Massaga.

Alisema Hospitali ya Bugando kwa sasa iko katika maandalizi ya kuelekea kilele cha kuadhimisha miaka 50 tangu kuanzishwa kwake mwaka 1971.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, akizungumza katika ziara hiyo ya balozi, alisema lengo lake ni kufuatilia miradi ambayo serikali ya Marekani imesaidia kupitia ubalozi wake nchini.

"Haya mambo ni ya kimapinduzi unamfundisha mtu na unampatia nyenzo ya kuinuka moja kwa moja, hivyo kuna haja ya kushukuru ubalozi kwa ushirikiano wa kipekee kati ya taifa letu na Marekani," alisema.

Aliongeza kuwa msaada huo ni muhimu kwa kuwa umesaidia kupata maabara ya kisasa ambayo itakuwa na uwezo wa kupima magonjwa yote ikiwamo UVIKO -19.

Balozi wa Marekani nchini, Dk. Donald Wright, akizungumza baada ya kutembelea maabara ya kisasa ya hospitali hiyo, alisema nchi yake itaendelea kudumisha uhusiano wake na Tanzania.

Alisema lengo la uhusiano huo ni kuhakikisha wananchi wa Tanzania na mikoa ya Kanda ya Ziwa wanaendelea kunufaika na kuwa na afya njema.

"Serikali ya Marekani imekuwa ikisaidia serikali ya Tanzania kwa miaka mingi na imedhamiria kuboresha afya za Watanzania pamoja na kuimarisha uhusiano, kupambana na malaria, kifua kikuu, HIV, uzazi wa mpango, ebola na magonjwa mengine," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la MDH, Dk. David Sando, alisema kupitia ufadhili wa Marekani wameboresha maabara ya hospitali ambayo kwa sasa inaweza kupima UVIKO-19 na kupata majibu kwa saa 24.

Alisema kabla ya kuboresha maabara hiyo, watu waliopimwa UVIKO -19 kwa kanda ya ziwa sampuli zao zilitumwa mkoani Dar es Salaam na kulazimika kusubiri majibu kwa siku 3, lakini kwa sasa kila kitu kitafanyika hapo.

# TAKUKURU yafuatilia bil. 14/- za madarasa

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Morogoro, imeanza kufuatilia Sh. bilioni 14. 1, zilizotolewa na serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 707 kwa halmashauri zilizopo Mkoa wa Morogoro, kwa ajili ya wanafunzi wanaotarajia kujiunga na kidato cha kwanza mwakani.

Mkuu wa TAKUKURU mkoa huo, Manyama Tungaraza, aliyasema hayo wakati akitoa taarifa ya utendaji kazi wa taasisi hiyo kwa umma kipindi cha kuanzia Julai hadi Septemba 2021.

Alisema Oktoba hadi Desemba 2021, imejiwekea mikakati mbalimbali ikiwa na ufuatiliaji wa fedha hizo zilizotolewa kwa halmashauri zote tisa kulingana na mgawanyo wa mahitaji husika. Pia, alisema kwa serikali kutoa fedha hizo ni muhimu kwa watendaji waliopewa dhamana ya kusimamia ujenzi wa madarasa, kuhakikisha shilingi ya mwisho inatumika ipasavyo.

Tungaraza alisema hatua kali zitachukuliwa kwa wote, ambao kwa namna moja au nyingine wamejipanga kuzifanyia fedha hizo ubadhirifu fedha hizo zilizotolewa naserikali, kwa ajili ya Watanzania maskini wenye kiu ya kupata huduma bora ya elimu.

Tungaraza aliwataka wananchi kwenye maeneo ya miradi mbalimbali kufuatilia kwa karibu, kulinda vifaa kwa kuwa ni kwa faida yao na serikali imewapunguzia mzigo wa kuchangia ujenzi.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**OMBI LA KUONESHA NIA KWA AJILI YA UTOAJI WA HUDUMA YA SAMANI ZA OFISI PAMOJA NA UWEKAJI WA SAMANI KATIKA OFISI**
**KUMBUKUMBU 0010007217**

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V. inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma ya uwekezaji wa vyombo vya ofisini.

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA:**

- EACOP inahitaji huduma kutoka kwa mtoa huduma mwenye uzoefu na sifa nzuri ya kutoa huduma za samani za ofisi pamoja na kuziweka katika ofisi ipasavyo.
- Madawati na meza za kufanyia kazi (vituo vya kazi vinavyoweza kuongezwa na kupunguzwa urefu wakati wa matumizi).
- Meza na viti vya vyumba vya mikutano (kiwango cha kawaida na kiwango cha vyumba vya mikutano).
- Viti vya ofisini vinavyoweza kurefushwa au kufupishwa na vilivyo undwa kwa ajili ya kutoa usaidizi bora kwa mgongo wakati wa kukaa (ergonomic).
- Makabati ya kuhifadhi mafaili (Credenzes).
- Kabati za kuhifadhi vitu mbali mbali.

**VIGEZO MUHIMU:**

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

- Uthibitisho wa Uzoefu, utendaji, na uwezo katika kutekeleza kazi zilizoainishwa katika mawanda ya kazi, kwa viwango vya juu nchini Tanzania, kwa kufuata viwango vya kitaifa na kimataifa (ikiwa ni pamoja na Viwango vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC), na uzoefu wa angalau miaka 5 katika utendaji wa huduma kama hizo ndani ya Tanzania au Kimataifa.
- Uthibitisho wa watendakazi husika wenye vigezo na uzoefu katika uwekaji wa samani katika ofisi.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji namsambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutekeleza shughuli za progamu.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani.
- Uwezo wa kifedha kuweza kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha mahesabu ya fedha ya mwaka 2017.

- Uthibitisho wa sera ya ndani ya Afya, Mazingira na Usalama, taratibu na mchakato kulingana na viwango vya ndani vya viwanda vya kazi husika.
- Uthibitisho wa usajili katika mamlaka husika ndani ya nchi kwa ajili ya utoaji wa huduma husika.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao kwa lugha ya kiingereza pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacoptz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11 jinni** za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **....Novemba 2021.** Kichwa cha Habari cha barua pepe kiwe ni kumbukumbu namba husika tu. Kichwa cha Barua Pepe kiwe ni **0010007217.**

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia iii kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo iu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonyesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

216552602

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Elimu ichangamkiwe Wiki Huduma Fedha

**SERIKALI** imeanzisha maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Fedha kitaifa ukiwa ni utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha wa mwaka 2020/21-2029/30 kupitia elimu ya umma ambayo ni moja ya maeneo ya kipaumbele katika utekelezaji wa mpango huo.

Hivyo katika hatua za utekelezaji, Wizara ya Fedha na Mipango imeandaa programu ya kutoa elimu ka umma ya mwaka 2021/22-2025/28. Programu imeweka mikakati ikiwamo matukio na mbinu zitakazotumika katika utoaji wa elimu ya fedha kwa umma.

Moja ya mikakati hiyo ni kuwapo kwa maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Fedha kila mwaka ambapo elimu ya fedha itakuwa inatolewa kwa wananchi kupitia njia mbalimbali.

Katika utekelezaji wa programu ya utoaji elimu wa masuala ya fedha, serikali inakusudia ifikapo mwaka 2025 takribani asilimia 80 ya wananchi watakuwa wamepata uelewa wa masuala ya fedha, kutokana na utafiti kuonyesha kuwa uelewa bado ni mdogo.

Kwa mujibu wa utafiti huo wa Finscope nchini wa mwaka 2017, ni asilimia 48.8 tu ya nguvu kazi ndio waliotumia huduma rasmi za fedha, hivyo kubaki na kundi la Watanzania ambao hawafaidiki na huduma hizi, hivyo kukosa fursa za kuboresha maisha yao kupitia shughuli mbalimbali za kiuchumi na hatimaye kuchangia katika kukuza Pato la Taifa.

Tunaona kwamba mkakati huu hususani wa kuanzishwa Wiki ya Huduma za Fedha ni njia yenye tija katika kufikisha elimu ya masuala ya fedha kwa kundi kubwa la Watanzania tukiamini kuwa itajenga uelewa na weledi katika matumizi sahihi ya huduma za fedha.

Pia itawezesha kuimarisha ufanisi wa masoko ya fedha kupitia elimu ya fedha, kuongeza upatikanaji huduma za fedha, kutoa elimu ya kuwezesha kumlinda mtumiaji wa huduma za fedha na kuwezesha wananchi kusimamia vizuri rasilimali fedha.

Kadhalika, itasaidia kuwezesha wajasiriamali wadogo kuongeza ujuzi na matumizi sahihi ya huduma za fedha katika kukuza biashara zao, kuimarika kwa utamaduni wa kujiwekea akiba, kukopa na kulipa madeni na kuongezeka kwa mchango wa Sekta ya Fedha kwenye ukuaji wa uchumi.

Kwa kuwa maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Fedha yamefanyika kwa mara ya kwanza mkoani Dar es Salaam kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja kuanzia Jumatatu hadi Novemba 14, tunawahamasisha wananchi wajitokeze kwa wingi kwenda kupata elimu ya masuala ya fedha ili wanufaike kiuchumi. Kwa kufanya hivyo, watapata uelewa wa masuala ya mikopo, uwekaji wa akiba, kuwekeza na matumizi sahihi ya fedha kutoka kwa watoaji wa elimu.


Ni matarajio yetu kuwa matokeo ya kuadhimishwa Wiki ya Huduma za Fedha yatakuwa chanya kwa watu binafsi, kaya, jamii na taifa kwa ujumla kwa kuongeza idadi ya watu wenye kiwango cha ufahamu elimu ya fedha na maarifa juu ya upatikanaji na utumiaji wa bidhaa na huduma rasmi za fedha.

Vilevile, kuimarika kwa matumizi ya masoko ya fedha, kusogeza huduma za fedha karibu zaidi na wananchi na kuhamasisha matumizi ya huduma hizo, kuwaunganisha wajasiriamali na fursa zinazotolewa na sekta ya fedha katika kukuza na kuimarisha biashara zao.

Elimu hii pia itawawezesha wananchi kupata maarifa na uelewa wa masuala ya fedha, hivyo kuwezesha kujenga utamaduni wa kutumia huduma rasmi za fedha na kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Mashaka Mgeta

## Muungwana Lazima Nilonge

# Malima, Makongoro waigwe ukomavu kero za mipakani

**WAKUU** wa mikoa ya Tanga na Manyara, Adam Malima na Makongoro Nyerere, wametumia kila lililowezekana kumaliza utata wa mpaka kati ya mikoa hiyo, wakiwashirikisha wataalamu wa ardhi na upimaji.

Wamefanya ziara iliyowafikisha eneo lenye urefu wa kilomita 420 wakikagua alama za mipaka, kupata ufafanuzi kutoka kwa wataalamu, kuwasikiliza na kujibu maswali ya wananchi waliojitokeza kuwalaki kwenye baadhi ya maeneo. Lengo ni kutimiza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan, kuwataka wakuu wa mikoa hao, kama ilivyokuwa na wengine kutatua kero za wananchi hususani zinazohusiana na masuala ya ardhi na mipaka.

Tangu kutolewa kwa agizo hilo Mei 19, mwaka huu, walipoapishwa wakuu wa wilaya, Malima na Makongoro wamejitokeza hadharani kushiriki ziara ya pamoja, ikiwa ni baada ya kufanya kikao mkoani Manyara, kilichokuwa mahususi kushughulikia mpaka kati ya mikoa hiyo.

Wawili hawa wameonyesha nia ya kulivusha taifa katika kukabiliana na kutatua changamoto zinazowagusa wananchi za umiliki wa ardhi ambazo husababisha uhasama. Malima na Makongoro wamejitokeza kuwa kielelezo cha utimilifu wa dhana ya uongozi unaojali na kushughulikia kero zinazowasumbua wananchi baada ya

'kuweka kambi' mjini Kilindi, mahali penye miundombinu inayoendelea kukua na kuboreshwa, wakichangamana na wananchi wa kawaida hadi maeneo ya vijijini, kujadiliana namna bora ya kupata ututuzi wa kero za mipaka.

Wawili hao wakiwa na msafara wenye wakuu wa wilaya, makatibu tawala wa wilaya, wakurugenzi watendaji wa halmashauri za Kilindi, Kiteto, Handeni na Simanjiro, wakafikia alama za mipaka na kubaini mambo ambayo kama ziara hiyo isingefanyika, bila shaka kiwango cha uelewa kuhusu kadhia hiyo kisingekuwa kwa ukubwa uliopo sasa.

Uelewa wa asili na muundo wa changamoto zinazoikabili jamii, ni miongoni mwa mambo msingi yanayowezesha ufanisi katika mchakato wa kupata suluhu ya kudumu, hivyo ni dhahiri hatua inayotekelezwa sasa na Malima na Makongoro ni ya kuigwa, kuwezeshwa zaidi na kuungwa mkono.

Ndiyo maana katika kikao cha majumuisho ya ziara hiyo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kilindi, Idrisa Mgaza, anasema mfumo wa utatuzi wa mgogoro wa mpaka unaotumiwa na Malima na Makongoro haujapata kuonekana tangu kuibuka kwa utata wa mpaka katika maeneo kadhaa yanayoitenganisha mikoa hiyo.

Anasema zipo dalili njema zinazoonyesha kufikiwa kwa suluhu ya kudumu, huku akitoa rai kwa wanasiasa hasa wanaotokana na kuchaguliwa na wananchi, kutokuwa sehemu ya vyanzo vya kuchochea migogoro inayohusisha ardhi na mipaka.

Mgaza anaungwa mkono na wenyeviti wa halmashauri za Kiteto, Abdallah Bundala na wa Simanjiro, Taiko Laizer ambaye 'anawanyooshea kidole' viongozi wa baadhi ya vijiji vilivyopo mpakani, kwa kuuza ardhi nje ya maeneo yao, jambo ambalo ni kinyume cha sheria na taratibu.

Laizer anasema, "pamoja na dalili za uchochezi unaofanywa na wanasiasa, lakini wapo viongozi wa vijijini wanaouza maeneo yaliyo nje ya mipaka yao na hivyo kuwa chanzo cha vurugu kwa wananchi wetu."

Wakuu wa mikoa hao wanaipokea hoja hiyo na kutoa maagizo kwa wakuu wa wilaya zenye viongozi wanaotuhumiwa, kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria ili mwenendo huo ukomeshwe.

Madiwani wa kata zilizoko na maeneo ya Kitwai mkoani Manyara, Sakayo Michael na Michael Ole Sediyo wa Saunyi (Tanga) kwa niaba ya wenzao, wanasema ziara ya wakuu wa mikoa hao ni ishara ya dhamira ya Rais Samia kutatua migogoro katika maeneo tofauti.

Kutokana na hali hiyo, ni dhahiri wakuu wa mikoa, Malima na Makongoro wanastahili pongezi na kuungwa mkono kwa jitihada hizo.

## HABARI KITAIFA

# GST yashawishi Slovakia, China kuwekeza nchini

**Asteria Muhozya na**

**Abubakari Kafumba,** DUBAI

MTENDAJI Mkuu wa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST), Dk. Musa Budeba, ameishawishi Slovakia kuwekeza Tanzania kwenye uchimbaji au ununuzi wa madini ya viwandani yanayotumika katika kutengeneza vifaa vya teknolojia mbalimbali yakiwamo magari.

Dk. Budeba alimweleza Mkurugenzi wa Uchumi na Uwekezaji wa Kampuni ya Sario inayomilikiwa na serikali ya nchi hiyo, Egon Zorad, kuhusu uwapo madini hayo ambayo ni malighafi katika utengenezaji wa bidhaa mbalimbali za viwandani.

"Tumeona Slovakia imepiga hatua katika masuala ya teknolojia ambapo wanatengeneza magari yanayotumia haidrojeni na tumeona wametengeneza mifano ya ndege. Kwetu sisi kama sekta ni fursa kuwavutia waje kuwekeza kwetu kwa ajili ya kupata malighafi ya kutengeneza bidhaa zao kwa sababu vitu vyote tulivyoviona vinahitaji malighafi zinazotokana na madini kama nickel, shaba, rare earth elements, na graphite ambayo yote yako kwetu," alisema.

Alisema hayo wakati wa kikao na mwakilishi huyo aliyefika katika banda la Tanzania baada ya wataalam wa Tanzania kutembelea banda la nchi hiyo katika Maonyesho ya Kimataifa ya Expo 2020 Dubai. Walipata fursa ya kujionea teknolojia mbalimbali zinazozalishwa na Slovakia likiwamo gari linalotumia hydrojeni.

Kwa mujibu wa Zorad, gari hilo ambalo limetengenezwa kwa takriban miaka mitatu, limetengenezwa na vyuo vikuu vya nchini humo kwa kushirikiana na serikali na kampuni binafsi.

Wataalam wa Tanzania baada ya kutembelea banda hilo, walifahamishwa kuhusu namna nchi hiyo inavyojaribu kukuza teknolojia zake na kuhamia katika mifumo mingine ikiwamo matumizi ya magari yanayotumia umeme.

Pia Dk. Budeba alimhakikishia mwakilishi huyo kuhusu upatikanaji wa rasilimali za kutosha yakiwamo mazingira wezeshi ya uwekezaji na biashara yaliyopo nchini ikiwamo hali ya usalama na uwapo wa miundombinu ya kuwawezesha kufanya shughuli zao kikamilifu. Pia alimweleza nia ya Tanzania kuunganishwa na wawekezaji wengine wakubwa kutoka Slovakia.

Mbali na kuchimba na kununua madini, Dk. Budeba alimshawishi kuhusu kufikiria namna Slovakia inavyoweza kuanzisha kampuni ya uundaji magari nchini Tanzania kutokana uhakika wa upatikanaji wa rasilimali ambazo zitahitajika katika uundaji bidhaa hizo. Pia Dk. Budeba alimhakikishia kuwa tayari Tanzania ina kanzidata yenye taarifa za kutosha kuhusu uwapo wa madini hayo.

Zorad alishukuru kukutana na wizara na kufahamishwa kuhusu uwapo wa rasilimali hizo na kutaka kupatiwa taarifa za kutosha kuhusu masuala muhimu ya uwekezaji na biashara ya madini Tanzania ili pia kampuni hiyo iiunganishe Tanzania na kampuni zingine za Slovakia.

"Nataka sana Tanzania kuwa moja ya nchi tutakayoshirikiana nayo kwenye biashara na vyuo vyetu. Tumeelezwa kuwa nchi yenu iko kwenye nafasi nzuri kibiashara katika masuala ya madini. Slovakia tunaandaa mkutano wa wawekezaji na tunatarajia kualika angalau nchi moja kutoka Afrika na haina shaka itakuwa Tanzania," alisema Zorad.

Mbali na masuala ya madini, pia mwakilishi huyo alielezea nia ya Slovakia kutaka ushirikiano na vyuo vikuu vya Tanzania hususan kwenye masuala ya utafiti.

Dk. Budeba na maofisa wengine wa Wizara ya Madini walifanya mkutano kwa njia ya mtandao na mwekezaji kutoka China aliyetaka kuwekeza kwa kushirikiana Shirika la Madini la Taifa (STAMICO). Dk. Budeba alimuunganisha mwekezaji huyo na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa STAMICO kwa hatua zaidi.

Katika hatua nyingine, Mkurugenzi wa Banda la Tanzania kwenye Maonyesha ya Expo 2020 Dubai, Getrude Ng'weshemi, aliendelea kusisitiza ushiriki wa uhakika kama huu kwa sekta zingine ambazo zinatarajiwa kushiriki katika maonyesho haya ili kuhakikisha Tanzania inatumia vilivyo fursa zilizoko Dubai na kwingine duniani kupitia maonyesho hayo.



Ujumbe wa Tanzania na Slovakia katika Maonyesho ya Kimataifa ya Expo 2020 Dubai, ukiangalia gari linalotumia haidrojeni lililotengenezwa nchini Slovakia. **PICHA: WIZARA YA MADINI**


**AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**
**Company No. 22797**

the bank for your development

## NOTICE FOR CONVENING THE ANNUAL GENERAL MEETING AND EXTRA ORDINARY GENERAL MEETING

**A: ANNUAL GENERAL MEETING**

**NOTICE IS HEREBY GIVEN THAT THE ANNUAL GENERAL MEETING OF AKIBA COMMERCIAL BANK PLC SHALL BE HELD ON SATURDAY, 4TH DECEMBER 2021 AT DAR ES SALAAM SERENA HOTEL FROM 10:00 A.M. (EAT)**

**AGENDA:**

1.0 NOTICE, CONFIRMATION OF QUORUM AND ADOPTION OF THE AGENDA

2.0 TO CONFIRM THE MINUTES OF THE PREVIOUS MEETING

3.0 TO DISCUSS MATTERS ARISING FROM THE PREVIOUS MINUTES

4.0 TO RECEIVE THE CHAIRMAN'S STATEMENT

5.0 TO RECEIVE AND APPROVE THE FINANCIAL STATEMENTS FOR THE YEAR ENDED 31ST DECEMBER, 2020 TOGETHER WITH THE DIRECTORS' AND AUDITORS' REPORTS THEREON

6.0 TO RECEIVE REPORT ON THE BANK'S PERFORMANCE

7.0 TO RECEIVE UPDATE ON PROJECT OX

8.0 TO APPROVE THE RE-APPOINTMENT/APPOINTMENT OF NEW DIRECTORS AND ACCEPT RESIGNATION OF DIRECTORS

9.0 TO APPROVE THE APPOINTMENT OF EXTERNAL AUDITORS FOR THE YEAR ENDING 31ST DECEMBER, 2021 AND APPROVE THEIR REMUNERATION

10.0 TO SET DATE FOR THE NEXT ANNUAL GENERAL MEETING

11.0 CLOSING REMARKS

**B: EXTRA ORDINARY GENERAL MEETING**

**NOTICE IS HEREBY GIVEN THAT AN EXTRA ORDINARY GENERAL MEETING OF AKIBA COMMERCIAL BANK PLC SHALL BE HELD ON SATURDAY, 4TH DECEMBER 2021 AT DAR ES SALAAM SERENA HOTEL IMMEDIATELY AFTER THE ANNUAL GENERAL MEETING**

**AGENDA:**

1.0 NOTICE, CONFIRMATION OF QUORUM AND ADOPTION OF THE AGENDA

2.0 TO RECEIVE AND APPROVE THE PROPOSAL FOR RECAPITALIZATION OF THE BANK
- 2.1 TO RECEIVE AND APPROVE PROPOSAL FOR CONVERSION OF ORDINARY SHARE TO PREFERENCE SHARE
- 2.2 TO RECEIVE AND APPROVE PROPOSAL FOR AMENDMENT OF MEMORANDUM AND ARTICLES OF ASSOCIATION OF THE COMPANY
- 2.3 TO RECEIVE AND APPROVE PROPOSAL FOR ALLOTMENT OF PREFERENCE SHARES

3.0 CLOSING REMARKS

**NOTE:**

**A. PAPERS FOR THE MEETING**
Papers for the meetings will be available for collection at the Bank's Registered Offices from Monday, 29th November 2021 and at the venue on the date of the meeting.

**B. ANY OTHER BUSINESS**
Any other business to be discussed during the Annual General Meeting must be communicated to the Company Secretary not later than 10:00 a.m. (EAT) Saturday, 27th November 2021.

**C. OPTION TO JOIN VIRTUALLY**
Shareholders may join the meeting virtually if unable to attend physically, by sending an email to the Company Secretary to register their attendance and obtain meeting access before Thursday, 2nd December 2021. The meeting can be accessed virtually only by Shareholders who have registered their attendance in accordance with this notice.

**D. ATTENDANCE BY PROXY**
A Shareholder entitled to attend and vote at these meetings may, if unable to attend in person, appoint a proxy to attend and vote on his/her behalf in accordance with the provisions of the Articles of the Company.

The instrument appointing a proxy must be signed by the respective Shareholder.

The instrument appointing a proxy must be submitted to the Company Secretary at the Bank's registered office or via email by 10.00 a.m. (EAT) Thursday, 2nd December 2021.

**E. TRAVEL AND ACCOMMODATION**
Each Shareholder shall be responsible for the cost of their own travel and accommodation.

**F. OTHER INFORMATION**
Shareholders are reminded to confirm/update their personal information with the Company Secretary in order to update the Company Register.

**G. CONTACT DETAILS FOR COMMUNICATION**

**Company Secretary**
**Akiba Commercial Bank Plc**
**3rd Floor, Amani Place, Ohio Street**
**P.O. Box 669**
**Dar es Salaam**

**Tel: 0742 972 072 or 0677 152 000**
**Email:** cs@acbtz.com or niwaeli.mziray@acbtz.com

**By Order of the Board**

**Niwaeli Mziray**
**Company Secretary**
**10th November 2021**

**Distribution:** Shareholders - Akiba Commercial Bank Plc

**Invitees:** Board of Directors - Akiba Commercial Bank Plc
Senior Management - Akiba Commercial Bank Plc
External Auditors - KPMG
**Director, Banks Supervision Department - Bank of Tanzania**

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**OMBI LA KUONESHA NIA KWA AJILI YA UTOAJI WA HUDUMA YA KUNUNUA GARI MPYA NA AU KUKODISHA. KUMBUKUMBU: 0010007221**

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V. inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma ya uwekezaji wa vyombo vya ofisini.

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA:**

Mradi wa EACOP unahitaji watoa huduma wenye uzoefu na uwezo yakinifu wa kutoa huduma ya kununua gari mpya na au kukodisha:

- Magari ya kati (SUV), Magari madogo yenye uwezo wa kubeba abiria 5 ambazo zinaendeshwa kwa mfumo wa Automatic transmisión (makadirio ya idadi kuanzia 30 mpaka 50 kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia sasa).
- Kupatikana kwa magari aina ya Double Cabin 4x4 ambayo yana mfumo wa uendeshaji wa Automatic Transmission (makadirio ya idadi 30 hadi 80 kwa kipindi cha kuanzia sasa mpaka mwaka).
- Kutoa huduma ya matengenezo ya magari husika (Preventive and periodic), kujumuisha usimamizi wa matairi na ubadilishaji wake.
- Kuorodhesha matawi au washirika wake ndani ya Tanzania.
- Kutoa taarifa za gari husika kama zina viwango vya kiusalama vinavyolingana na NCAP.
- Kutoa taarifa ambazo zitaonyesha aina ya gari au modeli ambazo zinapatikana kwa sasa (Stock) na ambazo wanategemea kuingiza nchini katika kipindi cha mwaka ujao.

**VIGEZO MUHIMU:**

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

- Uthibitisho wa Uzoefu, utendaji, na uwezo katika kutekeleza kazi zilizoainishwa katika mawanda ya kazi, kwa viwango vya juu nchini Tanzania, kwa kufuata viwango vya kitaifa na kimataifa (ikiwa ni pamoja na Viwango vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC), na uzoefu wa angalau miaka 5 katika utendaji wa huduma kama hizo ndani ya Tanzania au Kimataifa.
- Uthibitisho wa watendakazi husika wenye vigezo na uzoefu katika kutoa huduma ya kununua gari mpya na au kukodisha.
- Inashauriwa, muoneesha nia atume maombi ya kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani.
- Uwezo wa kifedha kuweza kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha mahesabu ya fedha ya mwaka uliopita.
- Uthibitisho wa sera ya ndani ya Afya, Mazingira na Usalama, taratibu na mchakato kulingana na viwango vya ndani vya viwanda vya kazi husika.
- Uthibitisho wa usajili katika mamlaka husika ndani ya nchi kwa ajili ya utoaji wa huduma husika.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao kwa lugha ya kiingereza pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacoptz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11 jioni** za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **25 Novemba 2021.** Kichwa cha Habari cha barua pepe kiwe ni kumbukumbu namba husika tu. Kichwa cha Barua Pepe kiwe ni **0010007221.**

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia iii kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo iu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni.

# Matumizi gesi asilia yalivyookoa tril. 38/-

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA kipindi cha mwaka 2004 hadi Juni 2020, matumizi ya gesi asilia ya Mnazi Bay na Songo Songo yamesaidia serikali kuokoa zaidi ya Sh. trioni 38, ambazo zingetumika kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya mitambo ya umeme na ya viwandani.

Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, alibainisha hayo jana jijini Dodoma, alipokuwa akitoa taarifa ya mafanikio ya sekta ya nishati katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika.

Alisema, tangu kupatikana Uhuru, serikali imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali ya kuiwezesha sekta ya mafuta na gesi kuchangia ipasavyo katika maendeleo ya nchi.

Alisema mikakati hiyo ni pamoja na kugunduliwa kwa gesi asilia katika maeneo ya Songo Songo, Mnazi Bay, Mkurunga, Kiliwani Kaskazini na kina kirefu cha bahari.

"Aidha gesi iliyogunduliwa nchi kavu na kina kirefu cha bahari ni futi za ujazo trioni 57.54 mwaka 2021" alisema Mramba.

Alisema ugunduzi huo umewezesha kuanza kutumika kwa gesi asilia kama chanzo cha nishati hususani kwa kuzalisha umeme, viwandani, majumbani na kwenye magari.

Aliongeza kuwa hadi Oktoba, 2021 viwanda 52, jijini Dar es Saalam, mkoani Pwani na Mtwara vinatumia gesi asilia.

"Aidha, vituo viwili vya kushindilia na kujaza gesi asilia kwenye magari jijini Dar es Salaam na Mtwara vinafanya kazi," alisisitiza Mramba.

Vilevile, alisema matumizi ya gesi asilia yamesaidia kupunguza utegemezi wa uzalishaji wa umeme kwa kutumia nguvu za maji ambapo hadi Novemba, 2021 takribani asilimia 60 ya umeme unazalishwa kwa kutumia gesi asilia.

Kwa mujibu wa Mramba, hadi Machi, 2021 mapato yanayotokana na mauzo ya gesi yamechangia zaidi ya Sh. bilioni 208, katika mfuko wa mafuta na gesi kuanzia mwaka wa fedha 2016/2017 baada ya kukamilika ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam.

"Hadi Desemba, 2020 serikali imepata mapato ya zaidi ya Sh. bilioni 441 yatokanayo na kodi mbalimbali kuanzia mwaka 2015, baada ya kukamilika kwa mradi wa bomba la kusafirishia gesi asilia kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam," alisema.

Pia, alisema kupitia sekta hiyo, Shirika la Maendeleo ya Mafuta (TPDC), limelipa zaidi ya Sh. bilioni 10, katika mwaka 2018/2019 na mwaka 2019/20 likiwa ni gawio kwa serikali.

Kuhusu huduma ya umeme na nishati jadidifu, alisema huduma za umeme nchini zimeendelea kuimarika kutoka na jitihada mbalimbali zilizofanywa na serikali kuanzia awamu ya kwanza chini ya uongozi wa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Alisema wakati Tanzania inapata Uhuru ni mikoa miwili tu ya Tanga na Dar es Salaam ndiyo ilikuwa na huduma za umeme.

# Tanzania mwenyeji mkutano wa umeme

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO), limekuwa mwenyeji wa mkutano wa watendaji wa mashirika 11 yanayozalisha, kusafirisha na kusambaza umeme katika nchi za Afrika mashariki na kati unaofanyika jijini hapa.

Katika mkutano huo, wawakilishi wa kutoka nchi 11 katika ukanda wa huo, wamekutana kujadili namna ya kukabiliana, kutatua changamoto za upatikanaji wa nishati ya umeme wa uhakika wenye gharama nafuu kwa wananchi wa nchi wanachama (East African Power Pool).

Mkutano unalengo la kuziunganisha nchi wanachama kupitia kampuni zinazozalisha na kusafirisha na kusambaza umeme Afrika Mashariki .

Akizungumza kwenye mkutano huo, Mwakilishi wa TANESCO, Mhandisi Philipo Lalisa, ambaye ni Kaimu Meneja Uendeshaji wa Mifumo ya Umeme katika gridi ya Taifa, alisema muunganiko wa nchi hizo unasaidia namna ya matumizi mazuri ya vyanzo vya umeme katika nchi wanachama.

Alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye vyanzo vya aina mbalimbali za uzalishaji umeme.

Alisema serikali ya Tanzania kupitia TANESCO inaendelea na maandalizi kuwezesha kuongeza upatikanaji umeme katika ukanda wa Afrika Mashariki na TANESCO inaendelea na ujenzi wa njia kuu ya usafirishaji umeme wa msongo wa kilovolti 400 utakaoiunganisha na Kenya kwa upande wa kaskazini ambapo ndipo umoja huu wa Afrika Mashariki unafikiwa pia kwa upande wa kusini.

Alisema mradi huo utaiwezesha TANESCO kusafirisha umeme hadi Zambia kupitia Tunduma, jambo ambalo linaiwezesha nchi kujiunga pia katika umoja wa kampuni zinazouziana umeme kusini mwa Afrika, hivyo kuwezesha nchi kuuza umeme katika nchi za Afrika Mashariki na zile zilizo kusini mwa Afrika .

## Mamilioni yatumika kwa miradi ya maendeleo kijijini

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

SERIKALI ya Kijiji cha Vianzi, Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, imetumia zaidi ya shilingi milioni 120 za mapato ya ndani kutekeleza miradi ya maendeleo.

Hayo yalisemwa na Mtendaji wa kijiji hicho, Rodha Charles, wakati akisoma taarifa kwenye mkutano mkuu wa kijiji.

Alitaja matumizi ya fedha hizo za mapato ya ndani shilingi milioni 129.6 ni ujenzi wa vyumba vya madarasa vinne katika shule mpya za msingi za Chang'ombe na Honda na ujenzi wa ofisi mbili katika shule hizo.

"Aidha, nyingine zimepelekwa katika ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (ODP) kwenye zahanati yetu pamoja na ununuzi wa hekari 12.5 sambamba na madawati 50, na karavati mbili katika ujenzi wa barabara za vitongoji vyao," alisema.

Aliongeza kuwa wanakarabati na kununua viti vya ofisi katika kijiji chao na Kitongoji cha Kwajokoa, na kwamba

wanatarajia kutumia shilingi milioni 25 kwa ajili ya ujenzi wa soko la kijiji.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Maulid Jongo, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwapatia shilingi milioni 20 ambazo zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kwenye Shule ya Sekondari Honda.

## Wapima saratani matiti, tezi dume

**Na Christina Mwakangale**

WAKAZI wa Dar es Salaam 175, wamejitokeza kupata huduma ya vipimo bure iliyotolewa na Chama cha Waradiografia Tanzania (TARA), kubaini iwapo wana magonjwa, ikiwamo saratani na tezi dume.

Vipimo vilivyotolewa ni kupima dalili za awali za saratani ya matiti na uvimbe na tezi dume kwenye mikoa tofauti, ikiwa ni kuelekea maadhimisho ya Wiki ya Waradiografia Duniani, inayoadhimishwa ifikapo Novemba 8, kila mwaka.

Katibu wa chama hicho, Omary Msehwa, alisema upimaji huo ulifanyika kuanzia mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma, huku jijini Mwanza huduma ikitarajiwa kutolewa.

Msehwa alisema pia upimaji huo uliofanyika kwenye kliniki za vituo vya afya RADTECH Wilaya ya Ilala na Temeke, ulilenga kupima kongosho, tumbo na kwamba kati ya wakazi 175 waliopima sita walipatiwa rufani kwa uchunguzi zaidi na tiba.

"Mwanza vipimo vitatolewa Novemba 10, mwaka huu, ikiwa ni mkoa ambao tutafanya mkutano mkuu wa TARA kukutanisha wadau wa eneo hili. Chama hiki kinahusisha wataalamu wa sonografia, radiografia na radiotherapia," alisema Msehwa.

# Madiwani wanusa 'upigaji', wamkataa Meneja TARURA

**Na Anthony Gervas,** MAGU

MADIWANI Halmashauri ya Wilaya ya Magu, wamemweka kiti moto na kumkataa Meneja wa Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) wilayani humo, Mhandisi Peter Leonidas, baada ya kushindwa kuwasilisha taarifa ya fedha za ujenzi wa barabara Sh. bilioni 2.3.

Hatua hiyo ilifikiwa baada ya meneja huyo kudaiwa kuwadanganya madiwani hao kutoa taarifa za mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo namna zinavyotumika katika miradi hiyo, kwenye kata mbalimbali.

Mhandisi huyo anadaiwa kuahidi kila mara kupeleka taarifa hizo katika mkutano bila utekelezaji, jambo ambalo limewaudhi madiwani hao na kuchukua uamuzi wa kukataa kuendelea kufanya kazi katika wilaya hiyo.

Akiunga mkono hatua hiyo Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Mpandalume Simon, alisema mapendekezo ya kumwondoa mhandisi huyo katika Wilaya ya Magu na kumhamishia wilaya zingine ni sahihi kutokana kutoa taarifa ambazo hazitekelezi.

"Mapendekezo yote ya madiwani nayaunga mkono, mhandisi huyu hatufai sababu ameshindwa kuleta taarifa za mchanganuo wa fedha zinavyotumika kwenye miradi ya kutengeneza barabara, hii ni mara ya tatu," alisema Mpandalume.

Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni moja zimetolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya mpango kazi wa maendeleo, zinazotakiwa kutekeleza miradi ya barabara kwenye kata 11, huku Sh. milioni 500 zikitolewa kwa ajili ya kutengeneza barabara ya Sayaka-Bubinza, Kata ya Lubugu.

Aidha, Sh. milioni 800 zimetolewa na serikali katika bajeti ya kawaida ambazo pia zitatumika katika matengenezo ya barabara zingine, kwenye kata mbalimbali wilayani humo.

Diwani wa Kata ya Bujashi, Lucas Deleli, alidai kuwa fedha hizo zinafanyiwa mchezo wa sungura kutokana na madai ya kuwapo kwa upigaji, hali inayosababisha kushindwa kuleta taarifa za mchanganuo huo.

Deleli alisema barabara zinazotengenezwa na TARURA hadi sasa nyingi hazipitiki huku akidai mkandarasi kutoonekana eneo la ujenzi.

Diwani wa Kata ya Lutale, Ng'anabuta Enos, alidai barabara kutengenezwa bila kuwekwa mitaro na karavati jambo ambalo limewatia wasiwasi na kufikia uamuzi wa kumkataa mhandisi huyo. "Wewe kuanzia leo bye bye," alisema Ng'wanabuta.

Baada ya kuhojiwa na madiwani mhandisi huyo, alishindwa kujitetea na kuondoka kwenye mkutano huo huku wakimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Fidelica Myovella, kumwondoa mtumishi huyo.

Katika sakata hilo, Katibu Tawala wa wilaya hiyo, Menruf Nyoni, aliwapongeza madiwani hao kufikia hatua hiyo, ili kuwadhibiti watumishi wanaofanya udanganyifu katika miradi ya maendeleo ya wananchi.

"Asanteni madiwani kuyaona hayo barabara nyingi hazipitiki, lakini sijawahi kuona mhandisi huyo ameleta taarifa za mchanganuo wa fedha za miradi hii katika mikutano yenu, pamoja na kwamba kwenye ofisi ya mkuu wa wilaya analeta nakala huo ni udhaifu," alidai Nyoni.

Aliwataka madiwani kila kata wanapoona fedha za miradi ya maendeleo ya wananchi zinagubikwa na udanganyifu watoe taarifa mapema kwa serikali, ili hatua stahiki zichukuliwe.

Alisema kila diwani anatakiwa kujua idadi ya barabara zake zinazotakiwa kutengenezwa kupitia fedha hizo, zinatengenezwa kwa kiwango gani na muda wa kukamilika.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya ABSA, Abdi Mohamed (kulia), akizungumza na Mkurugenzi wa Pact Tanzania, Mariana Balampama, katika hafla iliyoandaliwa na benki hiyo kwa wateja wake wa kampuni na wafanyabiashara, jijini Dar es Salaama jana. Katikati ni Meneja Uhusiano wa benki hiyo, Neema Athanas. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanaotumikisha wenye ulemavu waonywa

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MAOFISA Ustawi wa Jamii katika halmashauri zote za Mkoa wa Morogoro kwa kushirikiana na wajumbe wa kamati za watu wenye ulemavu, kwenye ofisi za wakuu wa wilaya wameagizwa kupiga marufuku vijana wanaowatumia watu wenye ulemavu kupita mitaani wakiomba fedha za kukidhi mahitaji yao.

Ofisa Ustawi wa Jamii mkoani Morogoro, Jesca Kagunila, alisema hayo jana wakati wa kikao cha kujadili huduma zilizotolewa kwa watu wenye ulemavu kwa mwezi Julai hadi Septemba, mwaka huu na kuweka mikakati ya kuunda kamati za watu wenye ulemavu katika mkoa huo.

Kagunila alisema haikubaliki na ni kinyume cha sheria kwa vijana wenye nguvu za kufanya kazi kuwatumia watu wenye ulemavu kupita mitaani na katika kumbi za starehe kuomba fedha hali inayochangia kuongezeka kwa idadi kubwa ya ombaomba ndani ya mkoa huo.

Alisema hakuna sababu watu wenye ulemavu kutumika kama vitega uchumi kwa sababu serikali imetoa mwongozo wa kuwasaidia kwa kila halmashauri kutenga fedha asilimia mbili zinazotokana na mapato ya ndani kwa ajili ya kundi hilo.

Vile vile, aliwataka watu walio kwenye kundi hilo kuchangamkia fursa hiyo ya fedha zilizotengwa kwa kuunda vikundi, ili kupatiwa mikopo ya serikali isiyo na riba na kuendesha maisha zao.

Kwa upande wake, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya watu wenye ulemavu Mkoa wa Morogoro, Hassan Mikazi, aliwataka watu wenye ulemavu kutambua utu wao na kukataa kutumika kama kitega uchumi, bali wafuate taratibu zinazotolewa na serikali kwa kujiunga katika vikundi, ili wawezeshwe kimikopo.

Katika hatua nyingine Mikazi aliiomba serikali kuwachukulia hatua watu wanaowafanyisha watu wenye ulemavu kazi za ombaomba, ili liwe fundisho kwa wengine wanaotumia fursa hiyo kuwatumikisha.

Akichangia katika kikao hicho Mjumbe wa Kamati ya watu wenye ulemavu, Dk. Lucy Nkya, alisema liandikwe andiko maalum liwasilishwe kwa kamati ya ulinzi na usalama inayoongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela, ili atoe tamko rasmi kuwachukulia hatua watu watakaobainika kuombaomba.

Naye Mwenyekiti wa SHIWAVITA Mkoa wa Morogoro, Oskar Changala, alisema utafiti walioufanya hivi karibuni umebaini kuwapo idadi kubwa ya ombaomba wanaotoka katika mikoa mingine kwenda Morogoro na mara kadhaa amekuwa akiwachukulia hatua, lakini bado kuna ongezeko kubwa la watu hao.

# Mbunge aja na suluhisho la upungufu wa dawa

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum, Agnesta Lambert, amesema ili kupunguza tatizo la ukosefu wa dawa pamoja na kuiwezesha Bohari ya Dawa (MSD) kutekeleza majukumu yake, serikali inapaswa kuipatia Sh. bilioni 600 kutoka katika fedha za msaada wa Sh. trilioni 1.3 ilizopokea.

Septemba 8, mwaka huu, Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) liliridhia kutoa mkopo nafuu kwa Serikali Dola za Marekani milioni 567.25 (Sh. trilioni 1.3) kwa ajili ya kukabiliana na athari za ugonjwa wa corona.

Akichangia mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/23, Lambert alisema kutokana na deni la serikali inalodaiwa na MSD kuzidi kukua, inapaswa sehemu ya fedha hizo za msaada zielekezwa katika kumaliza deni hilo, ili MSD ijiendeshe kwa ufanisi.

"Nafahamu hivi karibuni tumepokea mkopo wa Sh. trilioni 1.3, ili kuondokana na aibu ya serikali kudaiwa na MSD pamoja na kusababisha kushindwa kutimiza wajibu wao itengwe Sh. bilioni 600 zipelekwa MSD," alisema Lambert na kuongeza:

"Kwanza, ikamalize deni la serikali inalodaiwa ambalo ni Sh. bilioni 230 zitakazobakia Sh. bilioni bilioni 363.93 zitakuwa ni mtaji kwa MSD kutekeleza majukumu yao."

Lambert alisema MSD ndiyo chombo pekee kinachonunua na kusambaza dawa na vifaa tiba hapa nchini.

Alisema taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ya Agosti 18, mwaka huu iliweka bayana jinsi ambavyo deni la MSD kwa serikali limekuwa ni changamoto kubwa na kusababisha taasisi hiyo kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Alisema deni la serikali inalodaiwa na MSD hadi Agosti 18, mwaka huu lilikuwa ni Sh. bilioni 269, baada ya PAC kuikalipia serikali Septemba, mwaka huu, serikali ililipa Sh.bilioni 39 na kubakiza deni la Sh. bilioni 230.

Lambert alisema mwaka 2018/19 deni la serikali kwa MSD lilikuwa Sh. bilioni 53.

"Sasa linganisha deni la Sh. bilioni 53 kwa kipindi hicho na deni la sasa la Sh. bilioni 269, unaweza kuona namna gani MSD walivyo na hali mbaya, hivyo maana yake Watanzania wana hali mbaya sana katika sekta ya afya," alisema Lambert na kuongeza:

"Nimesoma taarifa ya Kamati ya Bajeti, inasema kuwa MSD ina hali mbaya, hivyo inahitaji Sh. bilioni 363.39 ili iweze kufanya majukumu yake kwa ufanisi."




Ofisa Mkuu wa Huduma za Kifedha wa Tigo Pesa, Angelica Pesha, akizungumza na waandishi wa habari katika uzinduzi wa huduma mpya ya bima ya kidijitali kwa vyombo vya usafiri ijulikanayo kama Tigo Motor Insurance kwa kushirikiana na kampuni ya Bima ya Milembe, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa Milembe Insurance, Muganyizi Tibaijuka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tigo, Milembe kuvipa bima kidijitali vyombo vya usafiri

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya huduma za kidijitali Tigo Tanzania kwa kushirikiana na Kampuni ya Bima ya Milembezi wamezindua huduma mpya ya bima ya vyombo vya usafiri.

Huduma hiyo ijulikanayo kama TIGO MOTOR INSURANCE, itakayowawezesha wateja wa Tigo Pesa kukatia vyombo vyao vya usafiri bima na kukamilisha taratibu zote muhimu kidijitali kwa kutumia simu zao za mkononi popote pale watakapokuwa kupitia Tigo Pesa.

Bima hii itahusisha aina mbalimbali za magari kama madogo ya kubeba mizigo, pikipiki, bajaji, mabasi, malori, trekta, mashine za uchimbaji na mengineyo ambayo yamesajiliwa kwa matumizi ya kibiashara na binafsi.

Ofisa Mkuu wa Huduma za Kifedha Tigo Pesa, Angelina Pesha, akizungumza kwenye uzinduzi jana jijini Dar es Salaam, alisema:

"Takriban watu milioni 53.18 wanapata huduma za simu za mkononi Tanzania, lakini ni asilimia 13 tu ya watu wote wanapata huduma za bima. Lengo letu ni kuendeleza huduma za bima ya kidijitali kote nchini, hasa kwa wale ambao wamepata ugumu wa kufikia huduma hizi kupitia njia zilizozoeleka.

Sekta ya Bima Tanzania inaendelea kuonyesha fursa nyingi za upanuzi na ukuaji, hii imejidhihirisha kupitia ongezeko la taasisi mbalimbali zinazojihusisha na utoaji wa bima ambalo lina uwezekano wa kuongeza mahitaji ya bidhaa za bima kidijitali kupitia simu ya mkononi, na sisi kama kampuni inayojali wateja wake ndio maana tukaamua kuja na TIGO MOTOR INSURANCE ."

Pesha alisema ushirikiano wao na bima ya Milembe unalenga kuziba pengo la upatikanaji wa huduma za bima kwa kutoa suluhisho la kidijitali ambalo litapunguza gharama na kuongeza upatikanaji wa bidhaa za bima.

Alisema wanaamini kuwa zaidi ya wateja milioni 9 wa Tigo Pesa watatumia huduma hii mpya ya bima, ambayo inapatikana kwa urahisi na gharama nafuu.

Naye Muganyizi Tibaijuka, Ofisa Mtendaji Mkuu kutoka Milembe Insurance, alisema

Bima ya Milembe wakiwa waanzilishi wa huduma ya bima za kidigitali nchini maarufu kama 'BimaPap' wana imani kuwa kushirikiana na Tigo kunathibitisha kuwa ni hatua nyingine katika kuboresha ufanisi wa utendaji kazi na uhakikisho wa utoaji wa huduma bora kwa umma.

Alisema kwa sasa wateja wa Tigo Pesa watapata unafuu wa kuvihudumia vyombo vyao vya usafiri na kupewa hati muhimu za bima zao papo hapo kupitia simu zao.

Tibaijuka alisema aidha katika tukio la ajali ya gari ikiwa itawekewa bima kupitia Tigo Pesa, mteja atatakiwa kuwasilisha taarifa ya madai kidijitali pasipo kulazimika kutembelea ofisi zao na madai yake yataanza kushughulikiwa.

"Hii inadhihirisha mustakabali mzuri kati ya bima yetu na wateja wa Tigo Pesa," alisema Tibaijuka.

## Ndugai awang'ata sikio w/biashara

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SPIKA wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Job Ndugai, amewataka wafanyabiashara kujenga tabia ya uwaminifu kwenye shughuli zao kama kigezo pekee kitakachowajengea imani kwa serikali na jamii ili kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi.

Akizungumza kwenye hafla iliyoandaliwa na Chemba ya Wafanyabiashara, wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA) jijini Dodoma juzi, Spika Ndugai alisema serikali inataka kuona sekta binafsi imara na inayokua, lakini inazingatia uwaminifu na uwazi katika shughuli zake.

"Sisi kama Bunge tuna imani kubwa, serikali inapenda sana kuona sekta binafsi inakua na kutoa mchango stahiki katika maendeleo ya taifa...lakini kitu pekee ambacho tunategemea kuona kutoka sekta binafsi ni kuonyesha uwaminifu na kuwa wawazi katika shughuli mnazofanya, kwani kuna baadhi ya wafanyabiashara sio waaminifu," alisema Ndungai.

Mbali ya wito huo, Spika Ndugai aliwataka wafanyabiashara na wazalishaji kutengeneza bidhaa zenye ubora na viwango vya hali ya juu ili bidhaa za Tanzania ziweze kushindana kwenye soko la dunia na kulipatia taifa fedha nyingi za kigeni sambamba na uchangiaji ukuaji wa uchumi.

"Sisi kama Bunge tupo tayari kufanya kazi na TCCIA kupitia Kamati yetu ya Kudumu ya Viwanda, Biashara na Mazingira. Tunapenda kuona sheria na sera mbalimbali zinasaidia kukuza na kuendeleza biashara na kukuza ucchumi nchini," alisema.

Alisema Dodoma ni mkoa wa kimkakati ambao unaweza kuwekeza kwenye kilimo, viwanda vya kusindika na biashara hivyo kuiomba TCCIA kuhamasisha wafanyabiashara kuchangamkia fursa hiyo kuwekeza sambamba na azma ya serikali ya kujenga uchumi unaotegemea viwanda ifikapo mwaka 2025.

Rais wa TCCIA, Paul Koyi, alisema TCCIA imekuwa mstari wa mbele katika kutoa ushauri wa namna bora ya kukuza mitaji kwa wajasiriamali, wafanyabiashara, wenye viwanda na kilimo ili kuchochea ukuaji wa uchumi na ongezeko la ajira.


"Nalishukuru sana Bunge la Jamhuri ya Muungano kwa kuonyesha imani kubwa kwetu (TCCIA), tutaendelea kufanya kazi karibu na Kamati ya Bunge kwa manufaa na maslahi mapana ya taifa," alisema Koyi.

Safari ya gwiji Maalim Seif kisiasa

Ukurasa 13



Ukurasa 14



COLLIN LUTHER POWELL



UMOJA VYAMA VYA UPINZANI

# Mbatia kuviunganisha kunavyozua hisia tofauti


**Na Sabato Kasika**

WAKATI vyama vya upinzani vikitafuta namna bora ya kupata mafanikio kisiasa baada ya kushindwa kwenye uchaguzi mkuu uliopita, Mwenyekiti wa NCCR- Mageuzi, James Mbatia, anasema kuungana ndiyo mkakati pekee wa kuvivusha kikamilifu mwaka 2025.

Anaitaja mbinu ya kuunganisha vyama vyote vya upinzani na wapenda demokrasia ndani ya miezi sita ili viwe imara kuufikia uchaguzi mkuu wa 2025 na CCM iondoke madarakani kwa kuwa imeshindwa kuwasaidia Watanzania.

Anatamani kuona Tanzania inakuwa na CUF, CHADEMA, ACT-Wazalendo na NCCR -Mageuzi vilivyo imara ili viisambatarishe CCM.

"Nitakuwa tayari kuunganisha vyama vyote na wapenda demokrasia ndani ya miezi sita tuwe imara ili 2025 tuiondoe CCM," anasema hayo kwenye kongamano la siku 360 za madhila yaliyotokana na uchaguzi mkuu wa mwaka jana, lililoandaliwa na CUF, jijini Dar es Salaam, akigusia umuhimu wa vyama vya upinzani kuunganisha nguvu ili kukabili mikikimikiki ya CCM 2025.



James Mbatia ametangaza mkakati wa kuviunganisha vyama vya upinzani. **PICHA: MTANDAO**

### JE WANAMKUBALI?

Naibu Katibu Mkuu wa CUF, Magdalena Sakaya, anasema, chama hicho kiko tayari kuunganisha nguvu kama ambavyo Mbatia anashauri, lakini uwe ni muungano wenye maslahi kwa umma, si kwa ajili ya chama fulani.

Anasema, CUF inaamini katika ushirika na vyama vingine, akikumbushia kuwa hata kuanzishwa kwa Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA), ilisimamia, lakini baadaye ikaamua kujitoa, baada ya kubaini UKAWA ulilenga kukinufaisha chama fulani, si Watanzania.

"Hivyo muungano anaosema Mbatia, tuko tayari ili mradi unufaishe Watanzania wote.Utofauti wa itikadi za vyama hauwezi kusababisha vyama visiunganishwe bali tatizo ni ajenda iliyojificha ambayo huletwa kwa sura ya kuunganisha vyama na inapojitokeza husababisha kusambaratika."

"Tunaamini Mbatia ana nia nzuri na anayetamani ushirikiano wa vyama, lakini bahati mbaya ujanja unaoletwa na baadhi ya wenzetu ndiyo unaosababisha kila chama kusimama peke yake," anakumbusha Sakaya.

Anataja uchaguzi wa mwaka 2015 kuwa ushindi ulikuwa wazi, lakini ukavurugwa na baadhi ya vyama vilivyokuwa vimeungana na kuanzisha UKAWA na kwamba kipindi hicho wananchi walikuwa na mwamko na uelewa wa haki zao za msingi lakini hali hiyo ikatoweka kutokana na baadhi ya viongozi wa upinzani kuweka mbele yao maslahi binafsi.

### KUONDOA UBINAFSI

Ado Shaibu ni Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, akitoa maoni yake anasema, umoja wa vyama ni muhimu na unahitajika, lakini kwanza vianze kuheshimiana, kuvumiliana na kuondoa ubinafsi.

Anayataja kuwa ndiyo mambo ambayo yanatakiwa kuwekwa pembeni ili vyama vya upinzani viunganishwe na kuwa na nguvu kubwa za kuikabili CCM katika uchaguzi mkuu ujao na kuongeza: "Vyama viheshimiane, vivumiliane, kuondoa tofauti na ubinafsi kama njia mojawapo ya kupata urahisi wa kuungana na kufanikiwa kuiondoa CCM 2025," anasema Shaibu.

Anasema, uzoefu katika uchaguzi mkuu wa 2015 na 2020, kuna haja ya vyama vya upinzani kuungana, ila anachohofia ni mtindo wa vyama kutoheshimiana, kutovumiliana na ubinafsi na kwamba ndiyo wachawi wa upinzani.

Ado anasema vikiwaondoka, kisha akapatikana mtu wa kuviunganisha kwa uhakika wanaweza kufanya makubwa katika uchaguzi wa mwaka 2025, akisema hata sasa upinzani unaungwanishwa na ajenda kuu za kudai katiba mpya, tume huru ya uchaguzi na kutaka Mwenyekiti wa CHADEMA Freeman Mbowe achiwe huru.

Anasema, kwa kuwa ajenda hizo zinavigusa vyama vyote vya upinzani vyenye nia ya kuondoa CCM madarakani, zitumike kama mkakati wa kuviunganisha kwa ajili ya uchaguzi ujao.

### SHERIA IONDOKE

Doyo Hassan Doyo Katibu Mkuu wa Chama cha ADC, anashauri kwanza vyama vipambane na sheria ya vyama vya siasa iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2020 ilifutwe ili viwe huru kuungana.

"Kwa sasa si rahisi kuungana, kwani vinabanwa na sheria hiyo inayotaka kwanza chama kingine kifutwe ndipo wanachama wake wajiunge kwingine, ndiyo maana ninashauri vipambane ili ifutwe," anasema Doyo.


Kwa mazingira ya sasa si rahisi kuwa na muungano wa kuikabili CCM kutokana na sheria hiyo na pia hakuna ajenda ya pamoja ya vyama upinzani ambayo inaweza kuviunganisha, anasema na kuongeza , "ugumu mwingine ambao ninauona ni kila chama kuwa na itikadi na malengo yake katika siasa, hali hii inaweza kuwa kama ilivyotokea enzi ya UKAWA na kusambaratika."

### MBATIA HANA SIFA

Mchambuzi wa siasa, Godwin Gonde, anasema, wazo la Mbatia ni zuri, lakini hana ushawishi wa kuunganisha vyama, na kwamba anatakiwa aachie damu changa zifanye kazi hiyo kwa vile kiongozi huyo amekaa kwenye siasa muda mrefu na inatosha kuandaa vijana wapya ambao wanaweza kushawishi Watanzania na hata vyama vya upinzani kuungana na kufanikiwa kutimiza lengo hilo.

"Wapinzani wanaweza kumkubali kuwa ana uwezo wa kuwanganisha, lakini ukweli ni kwamba ameshapitwa na wakati, hana ushawishi kama alivyokuwa zamani, kwani zama za watu wa aina yake zimepita," anasema Gonde.

Gonde ambaye ni Mhadhiri wa Chuo cha Diplomasia, anasisitiza kuwa kizazi cha Mbatia hakiwezi siasa za sasa, badala yake kinatakiwa kuwa nyuma kikiangalia kinachoendelea na kutoa ushauri wanapoombwa.



Rais Samia Suluhu Hassan, ameruhusu kukosolewa lakini kwa staha. **PICHA: MTANDAO**

# Serikali inavyong'arisha demokrasia iliyofubaa

**Na Deogratias Mutungi**

MNYONGE mnyongeni lakini haki yake mpeni. Ndivyo ninavyoweza kusema nikirejea msemo wa Kiswahili , lakini nabadilisha namna unavyotumiwa kwani, mnyonge mkinyonga ataionaje haki yake?

Hivyo mnyonge asinyongwe na haki yake apate. Tunaukosoa uongozi wa awamu ya sita kadri tunavyoweza na serikali imeruhusu kukosolewa huko.

Hata hivyo, wakati tukifanya hayo yatupasa kurejea mahali tulipo sasa na tulipotoka miaka mitano iliyopita.

Kwa kujenga tafakuri ya picha ya mambo yalivyo sasa na siku zilizopita tunaweza kutoa hukumu kwa serikali ya awamu ya sita kwa mizania ya haki na ulinganifu.

Ni haki kikatiba kuhoji na kukosoa mamlaka za utawala, wala siyo kosa au hatia au kuchonganisha serikali na watu wake.

Katiba ya mwaka 1977, ibara ya 18, vifungu vidogo (a),(b),(c) na (d), vinawapa uwanja mpana raia kuhoji na kudadisi "haki ya uhuru wa mawazo" kwa kukosoa na kuwasilisha fikra mbadala kwa watawala.

Nia ikiwa kuwasahihisha na kuwakumbusha wajibu wao kiutendaji kwenye kuwahudumia Watanzania ambao ndiyo msingi wa mamlaka yote.

Itakumbukwa kuwa utawala bora ni pamoja na kupokea chanya fikra za watu wengine, ni kwasababu hakuna kiongozi aliyebora kifikra kuliko mawazo ya tabaka analoliongoza, hao ndiyo wenye nchi na maono kwa taifa lao.

Viongozi wengi wa kisiasa hupenda zaidi kusifiwa na si kukosolewa, hata hivyo awamu ya sita, imechagua kuruhusu kukosolewa pia, vyombo vya habari na bunge vimeruhusiwa kuikosoa serikali.

Lakini, kwa kutumia lugha ya staha, kwa muktadha huo kukosoa na kushauri kwa kuzingatia weledi wa hoja, staha na masahihisho chanya pale inapobidi kufanya hivyo, maana taifa hili na rasilimali zake ni mali ya raia wake.

Sasa ni wazi kuwa awamu ya sita inang'ara kisiasa na kidemokrasia imeshika hatamu, demokrasia iliyokuwa likizo ya lazima sasa imerejeshwa.

Ofisini, wengi wanafurahi kurejea kwa demokrasia iliyoadimika kwa kipindi kirefu lakini wachache wamenuna na kuvimba kwa sababu ya mazoea ya hulka zao za mabavu na unyanyasaji wa demokrasia.

Hata hivyo, wahenga walisema wengi wape kile wanachokistahili, ni nyakati za awamu ya sita kusigina pembeni wenye vimelea vya kukwamisha safari ya demokrasia kama taifa.

Wapambe hao wanafahamika kwa sura na maumbo yao wakemewe na kuwaogopa kama maadui wa kisiasa na wa demokrasia.

Waswahili husema kupanga ni kuchagua, bila hiyana awamu ya sita imechagua dhana ya kazi na demokrasia, bila shaka inatambua wazi kuwa maendeleo endelevu na uchumi imara wa nchi na kipato cha watu huongezeka na kuchochewa zaidi na uwepo wa demokrasia ya kisiasa inayotoa fursa za uhuru na haki katika ushiriki wa shughuli za kiuchumi kwa wananchi.

Kuibana demokrasia kwa kigezo cha kujenga nchi ni kuzalisha uhasama baina ya watu na serikali sambamba na maendeleo yao sababu ikiwa ni hofu ya uonevu kutoka kwenye mamlaka za kiserikali na taasisi zake.

Ni dhahiri kuwa kuibana demokrasia kwa maelezo ya kujenga nchi ni 'uovu' wa kisiasa na uzalishaji wa chuki na uhasama miongoni mwa jamii ya tabaka la watawaliwa na makundi ya vyama vya kisiasa yenye itikadi tofauti na watawala.

Demokrasia ya kweli na vitendo na iliyo komavu na endelevu kwa mifumo ya utawala dhidi ya watawaliwa unanogesha kasi ya ukuaji wa maendeleo ya watu na uchumi wa nchi, hii ni kwa mujibu wa utafiti wa kisiasa dhidi ya demokrasia ya kweli na maendeleo ya watu.

Watanzania kwa kiasi walipoteza matumaini ya uwepo wa demokrasia ya uwazi na ukweli zaidi ya propaganda za sera na falsafa za vitisho na hofu.

Pengine swali la kimantiki kutoka kwa msomaji wa andiko hili linaweza kujikita kuuliza na kutaka kupata majibu ni kwa jinsi gani taifa lilipoteza demokrasia yake?

Wachambuzi wengi wanakwepa kutoa muhtasari wa swali hili, lakini ukweli unabaki kuwa demokrasia na maendeleo ni sawa na pande mbili za sarafu ambazo haziwezi kutenganishwa.

Wengi wanajiuliza ni kwa jinsi gani taifa lilipoteza demokrasia yake? Najenga hoja, ifahamike kuwa demokrasia ni dhana pana kinadharia lakini hupoteza maudhui na upana wake pale mamlaka za watawala kisiasa zinapoamua kutumia dola kuminya na kufifisha kabisa uhuru wa watu na kuisigina katiba kwa matakwa na amri ya kundi la watu wenye maslahi katika ujenzi wa nchi kwa sababu ya mitizamo ya mawazo yao binafsi badala ya miongozo, sera, miiko na dira za kitaifa katika nadharia ya uongozi wa umma.

Tanzania na watu wake walianza kushuhudia viashiria vya wazi vya kubinya uhuru wa watu kwa mtindo wa uzalendo kwanza, kazi kwanza, maendeleo hayana chama, demokrasia ilifichwa kwenye kichaka cha siasa za kiitikadi za kuishi na kutenda kadri ya matakwa ya kujenga nchi kwanza.

Madhara ya hujuma ya demokrasia hapa nchini ni makubwa na athari zake hazina mfano.

Kukosoana na kupongeza kwa nia moja ya kujenga taifa kwa ubora maridhawa, bila kununa wala kuchukiana au kuviziana kwa sababu ya mawazo mbadala kuliondoka.

Watawala walitakiwa kutafakari na kuchukua hatua za kujisahihisha kulingana na maudhui.

Uzalendo kwanza, haki ya maendeleo, demokrasia na uhuru wa maoni baadaye inamaana vitu hivyo havistahili kukosekana, ni lazima viende pamoja.

Kutokwepo haki hizo ni kutengeneza 'sumu' ya kifikra ndani ya nafsi za watu hasa wananchi wanaotamani kusikika.

Awamu ya sita ameonyesha uwezo wa kuongoza kwa mbinu jumuishi za kifalsafa katika kuwahudumia Watanzania, wapo wasiotaka kuusema ukweli.

Upo utofauti mkubwa wa kiutawala na kimfumo baina ya awamu ya sita na ya tano.

Kuamini katika sera na falsafa ya watu wakae kimya ni kuweka ombwe la ukosefu wa demokrasia ya kweli na ambayo inaweza kuibua viongozi wasiojali kwavile hakuna wakuwasemea.

Lakini, awamu ya sita inatenganishwa na hayo kwa vile inasimama katika mstari wa maridhiano, haki, usawa na kusimamia demokrasia iliyotukuka kwa maslahi ya wananchi wote.

Ni kwa, mfumo huu wa utawala wa awamu ya sita ni rahisi wananchi kushiriki kwa hiari katika ujenzi wa maendeleo ya taifa lao kwa sababu ya uwepo wa demokrasia rafiki inayotoa haki na uhuru wa watu kuhoji na kukosoa serikali bila uwepo wa vitisho iwe ni kutoka serikalini au kwenye vyombo vingine vya dola.

Kisiasa hii ni hatua kubwa na inayokubalika kidemokrasia. Wanasiasa wa leo wakubali kuwa sasa ni enzi mpya za utawala wa awamu ya sita ni zama mpya, ambazo kila mmoja atafakari njia zake.

"Mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani" ndilo la kukumbuka kuwa wapo waliojisahaulisha kuwa ipo siku demokrasia itashika hatamu na kurudi nyumbani kwao na sasa demokrasia imerejea ulingoni.

**Maoni: dmutungid@yahoo.com**
**0717-718619**

# Safari ya gwiji Maalim Seif kisiasa

Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR

## • Ilianza na Jumbe kumalizika na Mwinyi
## • Ilikuwa mwiko kushindwa, kukata tamaa

LINAPOTAJWA jina la Maalimu Seif, mambo mengi yanaambatana nalo. Ndiye mwasisi wa maridhiano, mwafaka wa CUF na CCM. Amepitia kwenye mikono ya karibu viongozi wote, Abdul Jumbe , Rais wa pili wa Zanzibar, baada ya mauaji ya Sheikh Abeid Amani Karume, ndiye aliyemuingiza katika siasa, Baba wa Taifa Julius Nyerere, akamkaribisha CCM wakati mstaafu Ali Hassan Mwinyi, alimuamini katika mageuzi ya kiuchumi, lakini Dk. Ali Mohammed Shein, akiwa Rais wa Zanzibar, hakumuacha akamchagua kwa mara ya kwanza Makamu wa Kwanza wa Rais.

Seif Sharif Hamad, hajasahaulika yuko kwenye fikra za Watanzania, wiki iliyopita zilifanyika kumbukizi za kiongozi huyo, aliyekuwa Makamu wa Kwanza Rais na Mwenyekiti wa chama cha ACT-Wazalendo.

Maalim Seif mwasisi wa mageuzi ya kisiasa ya maridhiano yaliyomaliza siasa za chuki na uhasama Zanzibar , aliyefariki Februari mwaka huu anakumbukwa kwa mengi.

Baada ya kumaliza shule ya sekondari aliajiriwa akiwa mwalimu na huo ukawa mwanzo wa jina la "maalim", hayo yanajiri mwaka 1963, alipohitimu na kuanza kufundisha shule mbalimbali Unguja na Pemba kabla ya kuingia katika siasa na jina hilo kupata umaarufu mkubwa.

Hadi anafariki dunia Februari 17, 2021 alibakisha cheo cha ngazi moja tu ya kuwa rais ambacho alikitafuta kwa miongo mingi lakini bila mafanikio kwani mtu hapati akitakacho bali kile anachojaaliwa.

Safari ya kisiasa ya Maalim Seif ilianzishwa na mwalimu wake katika Shule ya Lumumba, mstaafu Aboud Jumbe Mwinyi, aliyemteua kuwa katibu myeka (msaidizi binafsi) Ofisi ya Rais Ikulu.

Enzi Talib ni mwandishi mbobezi aliyefanyakazi na Rais Abeid Karume, anasema nyota ya Maalim Seif iling'ara kuanzia hapo na kwamba alipanda ngazi hadi alipochaguliwa kuwa Waziri wa Elimu kwenye serikali ya Jumbe mwaka 1982.

Maalim Seif alichaguliwa kuwa Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar akiwa amepanda ngazi zaidi ,baada ya Jumbe kujiuzulu 1984, Ali Hassan Mwinyi, alichukua usukani wa kuongoza Zanzibar, kabla ya kuchaguliwa kuwa Rais wa Tanzania mwaka 1985, Hamad anasifika kuwa alifanya kazi kikamilifu na Mzee Mwinyi na kuleta mageuzi makubwa ya kiuchumi na kufunguwa milango ya uwekezaji ikiwemo sekta ya biashara visiwani Zanzibar.

Waziri mstaafu wa Mipango na Uchumi, katika serikali ya mstaafu Mwinyi, Mohamed Fakih, anasema katika kipindi cha mwaka mmoja kazi kubwa ilifanywa ikiwamo kufungua milango ya uwekezaji na biashara likaanza jina la "Zanzibar ni njema atakaye aje". Baada ya Mwinyi kuwa Rais wa Tanzania, Maalim Seif, alianza safari ya kuwa Rais wa Zanzibar, ulikuwa wakati wa uchaguzi ndani ya chama ulioitishwa kuziba nafasi ya Mwinyi, Maalim Seif akishindwa na Idriss Abdull Wakil, aliyeibuka kuwa Rais wa Zanzibar wa awamu ya nne. Hakumuacha akaendelea kumchagua kuwa Waziri Kiongozi kwa mara nyingine.

Katika kipindi cha uongozi wa Idriss Abdull Wakil, misukosuko mingi ya kisiasa iliibuka na matokeo yake Maalim Seif pamoja na viongozi wenzake tisa walifukuzwa CCM kwa madai ya kutaka kusababisha uasi mwaka 1988.

"Maalim Seif alikuwa kiongozi hodari, mbunifu mwenye kipaji cha hali ya juu, ndiyo maana Mwalimu Nyerere alivutiwa na kumuingiza CCM, akishika nafasi ya Katibu Idara ya Mipango na Uchumi ya Sekretarieti ya CCM mwaka 1977 hadi 1987 wakati huo mstaafu Salmin Amour akiwa chini yake,"anasema Talib.

Maalim Seif ndiye bingwa wa vuguvugu la kisiasa la mfumo wa vyama vingi ambapo baada ya kufukuzwa CCM hakunyamaza alianza harakati za kuanzisha chama cha CUF, akiwa na timu ya wanaharakati vijana akiwamo Hamad Rashid Mohamed, Juma Duni, Juma Ngwali (sasa ni marehemu) pamoja na Soud Yussuf Mgeni, waliunda chama kuongoza siasa za mfumo wa vyama vingi ambao ulioanza rasmi 1992, anaongeza.

"Chama cha Wananchi CUF kilikuwa tishio kwa sababu katika kipindi hicho vuguvugu la kisiasa lilipambamoto na watu walikuwa wakitaka kuona mabadiliko makubwa ya kisiasa yanakuja"anasema Hamad Rashid Mohamed, aliyepata kuwa kiongozi mwandamizi wa chama hicho, lakini pia akiwa ni rafiki wa Maalim Seif kwa nyakati tofauti.

Uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi mwaka 1995 Maalim Seif alichuana vikali na mgombea wa CCM, Dk.Salmin Amour huku CCM ikipata upinzani mkali na ushindi mwembamba na huo kuwa mwanzo wa mgogoro wa kisiasa Zanzibar, uliotokana na madai wapinzani uibiwa kura zake, anaeleza.

Mgogoro uliibuka na viongozi wa CUF 18 wakashtakiwa kwa tuhuma za uhaini (kuipindua serikali), mwaka 1998 ambapo baada ya kusota ndani kwa miaka mitatu waliachiwa , mapema mwaka 2000 katika awamu ya mstaafu Abeid Amani Karume, anasema Hamad Rashid.

Mazungumzo ya maridhiano ya kisiasa ya mwafaka yalianza mwaka 1998 yakiongozwa na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola -mwanadiplomasia Chifu Emeka Enyauko, aliyewaleta pamoja viongozi wa CCM na CUF, kumaliza tofauti zao.

Hata hivyo mwafaka huo haukupata nguvu za kisheria na mara baada ya uchaguzi wa pili wa mfumo wa vyama vingi mwaka 2000 Zanzibar ilikumbwa na vurugu za kisiasa.

"Serikali ya Tanzania, iliyokuwa inaoongozwa na Benjamin Mkapa, iliingia doa la kisiasa la mivutano ya kisiasa na kuandika historia, "anasema Juma Duni Haji, mwanasiasa na mshirika wa Maalimu Seif.

Mwafaka wa pili ulitayarishwa na kuanzishwa kwa tume ya pamoja ya maridhiano iliyopewa jukumu la kufanya marekebisho ya sheria kuona maridhiano ya kisiasa yanakuwa na nguvu za kisheria ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kuondokana na siasa za chuki na uhasama, anasema Duni.

Yalipata nguvu za kisheria na ilipofika mwaka 2010 Wazanzibari walipiga kura ya maoni kuhusu mustakabali wa kisiasa na wananchi kwa asilimia 66.4 walitaka kuwapo kwa mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK), anaongeza.

Katika uchaguzi mkuu wa 2010 mgombea wa CCM Dk. Shein aliibuka na ushindi dhidi ya mpinzani wake Maalim Seif Sharif , ambaye alichaguliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mujibu wa maridhiano ya kisiasa yaliyotokana na mabadiliko ya katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 yaliyoidhinishwa kuanzishwa SUK.

Mwaka 2015 maalim Seif alishiriki katika uchaguzi mkuu akiwa Makamu wa Kwanza wa Rais, hata hivyo, matokeo ya uchaguzi huo yalifutwa na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) kwa madai ya ukiukwaji wa sheria na kanuni za uchaguzi .

ZEC iliitisha uchaguzi wa marudio lakini CUF iliususia kwa madai kwamba haikuona sababu za kushiriki na kutaka kuondosha shari zaidi zinazoweza kusababishwa na vyombo vya dola.

Maalim Seif hakukata tamaa licha ya CUF kukumbwa na mgogoro mkubwa wa kisiasa na yeye kujiondoa na kujiunga na ACT-Wazalendo aligombea tena urais kupitia chama hicho akichuana na Dk.Hussein Ali Mwinyi wa CCM, lakini akashindwa.

Mazungumzo ya kufikia maridhiano ya kisiasa na kuundwa SUK yalifanyika tena na maalim alikubali kuingia katika serikali na kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mujibu wa katiba ya Zanzibar, inayoelekeza kuwa SUK itaundwa kwa kushirikiana na chama kinachochukua nafasi ya pili na kupata asilimia 19 ya kura.

Maalim Seif aliitumikia SUK kwa takriban miezi minne kabla ya kufariki dunia Februari 17, 2021 na hapo kuhitimisha safari ya maisha na harakati za kisiasa na kiuongozi.



Maalim Seif katika harakati za kisiasa, alibakiza cheo kimoja cha kuwa rais. **PICHA: MTANDAO.**

# COLLIN LUTHER POWELL

## ■ Shujaa aliyeibeba, kuilinda Afrika
## ■ Alianika mauaji Dafur, uasi Angola



Collin Powell . **PICHA: MTANDAO**

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

WAZIRI wa zamani wa Mambo ya Nje wa Marekani, Collin Powell, aliyekuwa mtu mweusi wa kwanza kushika wadhifa huo, licha ya kufariki dunia hivi karibuni, ameiachia Afrika alama zisizofutika.

Aidha, ni kiongozi ambaye nyota yake iling'ara sana, alikuwa pia Mkuu wa Majeshi ya Marekani mwenye asili ya Afrika au mweusi na kuandika historia.

Akiwa na miaka 84, Powell alifariki Oktoba 18, mwaka huu, kutokana na changamoto za upumuaji za COVID-19.

Baada ya kustaafu jeshi, akiwa na cheo kikubwa aliteuliwa na Rais George W Bush kuwa Waziri wa Mambo ya Nje, mwaka 2001.

Jenerali huyo wa jeshi mwenye nyota nne ni mzaliwa Harlem jijini New York, Aprili 5, 1937. Wazazi wake wakiwa wahamiaji kutoka Jamaica.

Collin Powell anatajwa alikuwa mmoja kati ya Wamarekani weusi wenye nguvu sana kwa miongo kadhaa.

Marais watatu wa Chama cha Republican waliutambua uwezo wake mkubwa na kumteua kushika nyadhifa za juu na akafikia ngazi ya juu sana jeshini.

**MAJUKUMU SERIKALI**

Powell, alikuwa mshauri wa masuala ya usalama wa Rais Ronald Reagan kuanzia mwaka 1987 hadi 1989.

> “Jenerali huyo wa nyota nne na mwanachama wa Republican mwenye msimamo wa wastani alijaribu kugombea urais wa Marekani, akiwa wa kwanza mweusi kuonyesha nia mwaka 1996, lakini mke wake, Alma, alimshawishi kubadilisha uamuzi huo kwa kuhofia usalama wake.

Wakati wa vita vya Ghuba vya mwaka 1991, ambapo majeshi ya Marekani yaliyoongoza vikosi vya washirika kuyatoa majeshi ya Iraq nchini Kuwait, alikuwa ndiye mkuu wa majeshi chini ya Rais George Bush- (Baba).

Jenerali huyo wa nyota nne na mwanachama wa Republican mwenye msimamo wa wastani alijaribu kugombea urais wa Marekani, akiwa wa kwanza mweusi kuonyesha nia mwaka 1996, lakini mke wake, Alma, alimshawishi kubadilisha uamuzi huo kwa kuhofia usalama wake.

Mwaka 2008, akahitilafiana na msimamo wa chama chake na akamuunga mkono mgombea urais Democrat, Barack Obama, ambaye ndiye aliyekuja kuwa Mmarekani wa kwanza mweusi kuchaguliwa kuwa rais.

**ALIIBEBA AFRIKA**

Inawezekana kusema kuwa haijawahi kutokea kwa jinsi ambavyo Powell, alipenda kutatua matatizo ya Afrika hasa vita, umaskini, UKIMWI na VVU pamoja na kuweka utawala bora.

Mwaka 2001 aliizuru Afrika, akitembelea Uganda, Mali, Afrika Kusini na Kenya.

Ujumbe mkubwa ndani ya ziara zake ulikuwa Afrika ni kipaumbele cha Amerika, siyo eneo linalotakiwa kuachwa nyuma likishambulia na VVU na UKIMWI, si wakati wa kuendelea na vita na kuuana tena.

Ndizo zama za kuwa na utawala bora na kuachana na vita, machafuko na uasi pamoja na uongozi usio na demokrasia unaokandamiza wananchi, ndicho alichosisitiza.

> “Akiwa Waziri wa Mambo ya Nje aliyetembelea Afrika 2001, Powell hakutaka tena kusikia habari za vita na machafuko ya wenyewe kwa wenyewe yaliyokuwa yanaendelea Mali, Congo DRC, Liberia , Sudan na Angola.

Alikutana na Marais Alpha Oumar Konare wa Mali, Thabo Mbeki wa Afrika Kusini, Daniel arap Moi wa Kenya na Yoweri Museveni wa Uganda na kuahidi haya.

“Marekani itakuwa rafiki wa Waafrika wote wanaotafuta kuwa na amani. Lakini siyo Amerika inayotengeneza amani kwa Afrika...”

**AMEITIBU AFRIKA**

Collin Powell, alikuwa sehemu ya viongozi waliosimamia kuanzishwa Mfuko wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Kupambana na Malaria na UKIMWI (PEPFAR).

Mfuko huo ulisaidia kuandaa mikakati na kutoa rasilimali zilizowezesha kuwafikia mamilioni ya watu waliokuwa wameathirika kwa VVU na UKIMWI, walioumwa na kupewa dawa za kufubazi virusi na huduma nyingine.

**VITA DAFUR**

Mauaji ya kimbari yaliyokuwa yanafanyika katika Jimbo la Darfur lililoko Sudan Magharibi mpakani na Libya, Chad, na Central African Republic yasingefahamika bila Powell kuitangazia dunia.

Ndiye aliyelipua habari mpasuko za mauaji hayo yaliyohusisha askari waliokuwa wanaungwa mkono na Serikali ya Sudan wa Janjaweed waliowaua Wasudani weusi takriban 300,000, kujeruhi mamilioni na wengine maelfu kukimbia makazi yao.

Walitumia silaha za jadi za sime, fimbo pamoja na risasi na makombora kutekeleza azma hiyo.

Aidha, Powell na nchi yake ndiyo iliyofanikisha mchakato wa kuundwa taifa huru na changa duniani la Sudan ya Kusini baada ya kujitenga na Sudan mwaka 2011.

Akiwa Waziri wa Mambo ye Nje aliyetembelea Afrika 2001, Powell hakutaka tena kusikia habari za vita na machafuko ya wenyewe kwa wenyewe yaliyokuwa yanaendelea Mali, Congo DRC, Liberia , Sudan na Angola.

Angola ilikuwa na uasi na vita vilivyodumu kwa miongo kadhaa vikichochewa na Jonas Savimbi, vita hivyo vilikomeshwa Februari mwaka 2002 alipouawa Savimbi na Angola kubaki salama.

Ni katika uongozi wake uasi na vita vya wenyewe kwa wenyewe ulimalizika nchini Liberia na kumwondoa madarakani Charles Tailor, vita hivyo vilivyoanza mwaka 1989 vilimalizika 2003 na kufuatiwa na uchaguzi mkuu wa kidemokrasia uliomweka madarakani Sirleaf mwaka 2005, Rais wa kwanza mwanamke.

**KUPIGANIA MAENDELEO**

Ukaribu wa Collin Powell na Afrika, ulishuhudia kuanzishwa kwa Shirika la Changamoto za Milenia (MCC) lililofanikisha kuanzishwa miradi ya maendeleo na kuwekeza ili kupunguza umaskini kwenye bara hilo.

MCC ilianzisha miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ya ujenzi wa miundombinu barabara, nishati na maji.

Miradi hiyo baadaye ilifanikisha kufikishwa umeme na mkongo wa mawasiliano ya intaneti visiwani Zanzibar.

Pamoja na Tanzania mataifa mengine yaliyonufaika na Shirika la MCC ni Burkina Faso, kutatua matatizo ya kiuchumi na nishati. Mataifa mengine ni Benin, Ghana na Sierra Leone.



## Kamati Bunge yaipa tano LHRC

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kimepongezwa na Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria kutokana na kutoa maoni na mapendekezo yenye utafiti, ambayo yana mchango mkubwa katika kutungwa kwa sheria mbalimbali.

Pongezi hizo zilitolewa katika mkutano na wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria wakati wakichambua matokeo ya maoni ya wadau yaliyochukuliwa na ambayo hayakuchukuliwa kwa ajili ya kutumika katika kutungwa wa sheria.

Mwenyekiti wa Kamati Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, Emmanuel Mwakasaka ambaye aliongoza mkutano huo na LHRC kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, Najma Murtazar Giga, alisema, Bunge ni taasisi kubwa, lakini ni rafiki wa LHRC, hivyo limekuwa likipokea maoni mengi na kuyaingiza na kuyatumia katika kutunga sharia.

Alisema kama ikitokea maoni yameachwa basi ni kwa maslahi mapana ya taifa.

Mwakasaka alisema Bunge ni taasisi iliyojaa wataalamu wengi inatumia muda wake kupitia maoni na kujiridhisha katika kila jambo.

Mbunge wa Kiteto, Edward Ole Lekaite (CCM), alisema asilimia 47 ya maoni yaliyopokelewa na kuingizwa katika sheria ni mafanikio makubwa ya LHRC na hiyo inaonyesha kwamba kituo kinatao maoni yaliyofanyiwa utafiti wa kutosha.

Mbunge wa Manyoni Magharibi, Yahaya Massare (CCM), alisema, kiwango hicho cha mapendekezo kupokelewa na kamati na kuyatumia katika kutunga sheria ya nchi ni mafanikio makubwa ya LHRC.

"Kamati inawatia moyo mwendelee kutoa mapendekezo yaliyofanyiwa utafiti ambayo yanatoa mchango mkubwa katika sheria mbalimbali nchini," alisema.

Kwa upande wake, Giga alipongeza ushirikiano mzuri kati ya Kamati na LHRC ambao ulianza tangu katika Bunge la 11.

Giga aliihimiza LHRC, kuendelee kutoa maoni au mapendekezo ambayo yatatumika katika kutungwa sheria mpya au kufanyiwa marekebisho.

"Kama katika dirisha hili maoni au mapendekezo yamechukuliwa machache, basi mngoje katika dirisha lingine ili kutoa maoni yenu" alisema.

Awali Mratibu wa Mtandao wa Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu, Hilda Dadu, alipongeza Kamati ya Bunge kupokea maoni ya LHRC kwa asilimia hizo, na akaomba itoe nafasi zaidi kuhusu masuala ya usawa wa jinsia.

# Bilioni 149/- kukamilisha ujenzi wa hospitali za rufani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 149 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi kwenye hospitali za rufani katika kanda mbalimbali nchini.

Hospitali hizo ni ya Kanda ya Kusini Mtwara, Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (META), Hospitali ya Kanda ya Chato awamu ya kwanza pamoja na hospitali mpya za rufani za mikoa ya Njombe, Simiyu, Geita, Songwe, Katavi na Sekou Toure jijini Mwanza.

Pia Hospitali ya Manyara, Mara, pamoja na hospitali ya kumbukizi ya Mwalimu Nyerere (Kwangwa).

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alibainisha hayo juzi alipokuwa akitoa taarifa ya mafanikio ya wizara hiyo katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara.

Dk. Gwajima alisema lengo la kutenga kiasi hicho cha fedha ni kwenda kukamilisha shughuli za ujenzi ili kutoa fursa kwa Watanzania kupata huduma bora za matibabu katika maeneo yote nchini.

Aidha, alisema katika mapambano dhidi ya adui maradhi miaka kadhaa iliyopita baada ya Uhuru yamesababisha kuzaliwa kwa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM-2007-2017).

Alisema mpango huo umechangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa vituo vya kutolea huduma za afya nchi nzima na kusaidia kupungua kwa vifo vya watoto, kuongezeka kwa upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika vituo vyote, kuongezeka kwa udahili wa wanafunzi.

"Kuongezeka kwa ajira ya wataalamu waliopelekwa katika ngazi zote za vituo vya kutolea huduma katika halmashauri, mikoa, kanda na taifa," alisema Dk. Gwajima.

Alisema idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya ngazi zote imeongezeka hadi kufikia vituo 8,537 ikilinganishwa na vituo 1,343 mwaka 1960.

"Ongezeko hili ni sawa na asilimia 84.26, aidha kati ya vituo hivyo serikali inamiliki asilimia 64, mashirika ya dini asilimia 9 na vituo binafsi asilimia 27," alisema.

Kadhalika, alisema mtandao wa vituo vya huduma za afya umepanuka na kusogea karibu zaidi na wananchi ambapo, zahanati ni 7,242, vituo vya afya 926, na Hospitali za Wilaya ni 178, Hospitali zingine ni 151.

Vilevile hospitali za kibingwa ngazi ya mikoa ni 28, ngazi ya kanda sita, hospitali za ubingwa maalumu ni tano na hospitali ya taifa ni moja (MNH).

"Vituo vyote hivi vina jumla ya vitanda 90,488 ikiwa ni sawa na ongezeko la vitanda 71,656 sawa na asilimia 79.18. Kwa sasa uwiano wa vituo kwa idadi ya watu ni kituo kimoja kwa watu 6,751.5 (1: 6,751.5) tofauti na 1:40000-50000 kabla ya uhuru. Hivyo, Tanzania imefikia malengo ya umoja wa mataifa katika upatikanaji wa huduma za afya kwa kuzingatia idadi ya watu na jiografia.

"Mapambano dhidi ya adui maradhi baada ya uhuru yaliifikisha nchi kwenye kuanzishwa kwa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi ambapo kama nilivyosema awali hivi sasa tunazo hospitali 12 za ubingwa daraja la juu zinazotoa huduma ikiwamo, upasuaji mkubwa wa moyo, huduma za usafishaji na upandikizaji wa figo, matibabu ya kisasa ya saratani.

"Pamoja na matibabu ya mifupa na huduma nyinginezo nyingi ambazo zimepunguza rufani ya wagonjwa kwenda nje ya nchi na hivyo kuokoa fedha nyingi za kigeni ambazo zingetumika kuhudumia rufani hizo.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kulia) na Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, wakifuatilia michango ya wabunge kuhusu mwelekeo wa bajeti ya serikali ya mwaka 2022/2023/, bungeni jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Sababu mfumuko wa bei kubaki 4%

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MFUMUKO wa bei wa taifa kwa mwaka ulioishia mwezi Oktoba mwaka huu, umebaki kuwa asilimia 4 kama ilivyokuwa kwa mwaka ulioishia mwezi Septemba mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa Mkurugenzi wa Sensa ya Watu na Takwimu za Jamii kutoka NBS, Ruth Minja, alisema hali hiyo inamaanisha kuwa kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia mwezi Oktoba mwaka huu, imebaki kuwa sawa na kasi iliyokuwapo kwa mwaka ulioishia mwezi Septemba, mwaka huu.

Alisema, mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia mwezi Oktoba sawa na mfumuko wa bei wa mwaka ulioishia mwezi Septemba, mwaka huu umechangiwa na kuongezeka na kupungua kwa mfumko wa bei wa baadhi ya bidhaa za vyakula na zisizo za vyakula kwa kipindi kilichoishia mwezi Oktoba, 2021 zikilinganishwa na bei za mwezi Oktoba, 2020.

"Kwa mfano baadhi ya bidhaa za vyakula zilizoonyesha kupungua kwa mfumko wa bei mwezi Oktoba 2020 ni pamoja na maharagwe, kwa asilimia 5.5, dagaa (3.9), maziwa ya ng'ombe (5.1) na choroko (2.3)," alisema.

"Kwa upande mwingine bidhaa zisizo za vyakula zilizoonyesha kuongezeka kwa mfumko wa bei kwa mwezi Oktoba 2021 zikilinganishwa na bei za mwezi Oktoba 2020 ni pamoja na mavazi kwa asilimia 4.8, gesi ya kupikia (2.8), mkaa (3.9) na gharama za malazi kwenye nyumba za kulala wageni (5.7)."

Kwa mujibu wa Minja mfumko wa bei wa bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kwa mwaka ulioishia mwezi Oktoba 2021, umepungua hadi asilimia 3.9 kutoka 4.0 kwa mwaka ulioishia mwezi Septemba 2021.

Aidha, alisema, mfumuko wa bei ambao haujumuishi bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kwa mwezi Oktoba 2021 umebaki kuwa asilimia 4.1 kama ilivyokuwa kwa mwaka ulioishia mwezi Septemba, mwaka huu.

Kuhusu hali ya mfumuko wa bei kwa baadhi ya nchi za Afrika Mashariki kwa mwaka ulioishia mwezi Oktoba mwaka huu alisema, kwa nchi ya Kenya mfumuko umepungua hadi asilimia 6.45 kutoka asilimia 6.91 kwa mwaka ulioishia mwezi Septemba 2021, Kwa nchi ya Uganda alisema, mfumuko kipindi hicho umepungua hadi asilimia 1.9 kutoka 2.2.



# TFA yaiomba serikali shamba kuzalisha kilimo cha alizeti

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA cha Wakulima Tanganyika (TFA) kimeiomba serikali ikipatie shamba lenye ukubwa wa ekari 1,250 kwa ajili ya kilimo cha alizeti, ili kukabiliana na tatizo la uhaba wa mafuta ya kupikia nchini ambao unasababisha kutumia fedha nyingi kuagiza bidhaa hiyo nje ya nchi.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa TFA, Peter Sirikwa, aliyasema hayo wakati wa Mkutano Mkuu wa wanahisa wa chama hicho taifa uliofanyika jijini hapa.

Alisema wameshawasilisha ombi hilo katika Wizara ya Kilimo kwa maandishi na wanasubiri utekelezaji wake ili waitumie fursa hiyo kusaidiana na serikali kukabili tatizo la uhaba wa mbegu za alizeti nchini.

Sirikwa alisema ili kufanikisha jambo hilo wanaiomba serikali ikisaidie chama hicho kupata mikopo ya kawaida ili kizalishe mbegu bora kwa gharama nafuu na kuwawezesha wakulima kuzipata kwa bei nafuu.

"Lengo letu ni kuongeza upatikanaji wa mbegu bora za zao hilo hapa nchini ili kuongeza hata upatikanaji wa mafuta ya kupikia, tunataka tuzalishe mbegu hizo kwa bei nafuu ili na wakulima tuwauzie kwa bei nafuu," alisema Sirikwa.

Aidha, alisema chama hicho kinaendelea kushirikiana na serikali kuagiza pembejeo mbalimbali zikiwamo mbolea na viuatilifu kutoka nje ya nchi ili kuwarahisishia wakulima upatikanaji wa pembejeo hizo.

Vilevile, alisema chama hicho kimeshaanza kuzalisha pembejeo mbalimbali za kilimo ikiwamo mbolea zilizosajiliwa kwa jina la TFA na kuthibitishwa ubora wake na mamlaka ili kuwasaidia wakulima upatikanaji wa pembejeo.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alikipongeza chama hicho kwa ubunifu wa kutaka kuanza kuzalisha mbegu za alizeti ambazo zina mahitaji makubwa nchini.

Alisema Tanzania ina uhitaji mkubwa wa mbegu hizo ili kuongeza upatikanaji wa mafuta na kuondokana na tatizo la kuagiza mafuta ya kupikia nje ya nchi.

Homera alisema alizeti ni miongoni mwa mazao ya kimkakati ambayo serikali imeyawekea mkazo mkubwa wa kuongeza uzalishaji ikishirikiana na wadau mbalimbali wakiwamo wa sekta binafsi.

"Serikali inatumia zaidi ya Sh. bilioni 400 kila mwaka kuagiza mafuta ya kupikia nje ya nchi kiwango ambacho ni kikubwa sana, hivyo sisi kama serikali tutaangalia namna ya kushirikiana nanyi ili wazo lenu lifanikiwe," alisema Homera.

Alisema chama hicho ni muhimu kwa maendeleo ya taifa kutokana na kuwasaidia wakulima kupata pembejeo bora kwa bei nafuu na kwa wakati huku akiitaka TFA kuwasaidia pia wakulima kupata masoko ya mazao yao.

Makamu Mwenyekiti wa TFA, Cathy-Elizabeth Long'lway, alisema chama hicho kina jumla ya wanachama 5,000 lakini, walio hawazidi 1,500 kutokana na sababu mbalimbali.

Alisema baadhi ya wanachama hao walikata tamaa miaka ya nyuma wakati chama hicho kilipokuwa kinatengeneza hasara na kuwaomba kujitokeza kuendeleza hisa zao kwa kuwa sasa kipo vizuri.

Aliwataka wanahisa waliozeeka wawamilikishe watoto wao au ndugu wanaowaamini kwa kuwa kila mwanachama ana haki na hisa zake.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, akizungumza katika mkutano mkuu wa wanahisa wa Chama cha Wakulima Tanganyika (TFA), jijini Mbeya mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Waelezwa umuhimu kuandika wosia

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATENDAJI wa Wakala wa Usajili wa Vizazi na Vifo (RITA) wametakiwa kutoa elimu kwa wananchi wengi hasa wa vijijini kuhusu umuhimu wa kusajili vizazi na vifo na kuandaa wosia ili kuepusha migogoro ya kifamilia ambayo imekuwa ikiibuka mara kwa mara.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitoa agizo hilo juzi jijini hapa wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Sheria ambayo yameandaliwa na Wizara ya Katiba na Sheria na kufanyika kitaifa, Nzovwe jijini hapa.

Homera alisema wananchi wengi wa vijijini hawana uelewa wa kutosha kuhusu umuhimu wa kuandika wosi jambo linalosababisha migogoro kwa wanafamilia hasa wajane, wagane na yatima ambao huwa wanakosa haki zao.

Alisema RITA wanapaswa kutambua kuwa wana jukumu kubwa la kutoa elimu kwa wananchi kwa kuwa kuna ongezeko la matatizo ya kifamilia hasa kwa wanandoa na wakati mwingine kusababisha wanafamilia kufarakana.

"Hii elimu mnapotoa hakikisheni mnayafikia mpaka maeneo ya vijijini ambako ndiko kuna matatizo makubwa, tunapokea malalamiko mengi sana ya wanandoa hasa kinamama kuporwa mali zao baada ya waume zao kufariki," alisema Homera. Alisema wakati mwingine baadhi ya wananchi wa vijijini huwa hawaandiki wosia kwa sababu ya mila potofu ambazo wanapandikizana na kupotoshana na baadhi wanaamini kuwa kuandika wosia ni kujitabiria kifo.

Alisema wosia huwa unatakiwa kuainisha kila mali itamilikiwa na nani endapo mmiliki wa awali hatakuwapo na baada ya kufariki wanafamilia wanagawana mali kulingana na maelekezo ya marehemu jambo ambalo linapunguza migogoro.

Homera aliongeza kuwa mila na desturi zilizopitwa na wakati ni tatizo lingine ambalo husababisha migogoro kwenye familia na kuwataka RITA pia kupambana kuhakikisha zinakwisha.

Ofisa Msajili Msaidizi wa RITA, Joseph Mwakatobe, alisema taasisi hiyo ilipokea ushauri na maelekezo ya Mkuu wa Mkoa na kwamba watahakikisha wanazingatia kwa ajili ya kuongeza ufanisi kwenye utendaji wao.

Alisema lengo la taasisi hiyo ni kuhakikisha wanawafikia wananchi wengi zaidi bila kujali maeneo wanayoishi ili kuhakikisha elimu kuhusu umuhimu wa kuandika wosia na kusajili vizazi na vifo kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

"Maelezo ya Mkuu wa Mkoa yamelenga kwenye majukumu yetu ya kila siku na kupitia maadhimisho haya tutawafikia wananchi wengi zaidi na wa kila rika wakiwapo walio ndani ya ndoa," alisema Mwakatobe.

Nao baadhi ya wananchi waliohudhuria maonyesho ya maadhimisho hayo waliiomba RITA kuwafikia na kuwapatia elimu kuanzia ngazi za chini wakiwamo wanafunzi ili uelewa kuhusu umuhimu wa wosia uanze kujulikana mapema.

Maadhimisho ya Wiki ya Sheria yanatarajiwa kufikia kilele chake Novemba 12, wananchi wanafundishwa mambo mbalimbali kuhusu masuala ya sheria.

## Waomba kuboreshewa skimu ya umwagiliaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa kilimo cha umwagiliaji katika Bonde la Utengule, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani hapa, wameiomba serikali kuwaboreshea skimu ya umwagiliaji ya bonde hilo kwa kusakafia mfereji ili kupunguza upotevu wa maji.

Wakizungumza na Nipashe juzi, wakulima hao walisema chanzo cha maji cha skimu hiyo ambacho ni Mto Nzovwe kina maji mengi, lakini kutokana na mfereji huo kutosakafiwa yanapotea njiani na kusababisha upungufu kwenye mashamba.

Mmoja wa wakulima hao, Yohana Mwazyunga alisema, wakulima wamekuwa wakigombania maji mara kwa mara kutokana na kiasi kinachofika mashambani kutokidhi mahitaji na njia pekee ya kuondoa migogoro hiyo ni kuiboresha skimu.

Alisema wakati mwingine wanalazimika kuweka mgawo wa maji ili wakulima wamwagilie kwa awamu, lakini bado hayatoshelezi huku mwamko wa wakulima kulima kilimo cha umwagiliaji ukiongezeka.

"Huu mfereji una urefu wa zaidi ya kilomita 10, lakini ukisakafiwa angalau kilomita tano tatizo litakuwa limepungua kwa kiasi kikubwa, ukienda kwenye chanzo unakuta maji tuliyochukua ni mengi, lakini yanayofika huku mashambani ni kidogo sana," alisema Mwazyunga.

Naye Godlove Huruma, mwenyekiti wa kikundi cha vijana wanaolima vitunguu katika bonde hilo, alisema wakati mwingine wanalazimika kulala mashambani ili wamwagilie usiku wakati watumiaji huwa wachache.

Hata hivyo, alisema kwa sasa watu wengi wamegundua mbinu hiyo hali ambayo bado inasababisha migogoro ya kugombea maji huku akidai kuwa muda wa usiku hata usalama huwa ni mdogo.

"Humu mashambani ni hatari sana nyakati za usiku maana kama unavyojua huo ni muda ambao unaweza ukang'atwa na nyoka au hata kama una adui yako anaweza akautumia muda huo kukuvizia na kukudhuru," alisema Godlove.

Alisema baadhi ya wakulima wenye mitaji mikubwa wanatumia mashine kuvuta maji kutoka Mto Nzovwe, lakini kwa vikundi vya vijana kama cha kwao ambavyo havina mitaji inakuwa vigumu.

Katika hatua nyingine wakulima hao waliiomba serikali iwasaidie kupunguza bei ya mbolea ili kuepusha gharama za uzalishaji wakidai kuwa kwa sasa wananunua mbolea kwa zaidi ya Sh. 100,000 kwa mfuko wa kilo 50.



# Mwinyi aipongeza Ireland misaada

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi ameipongeza Ireland kwa kuahidi kuiunga mkono serikali ya anayoiongoza katika kuleta maendeleo.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana alipokutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Jamhuri ya Ireland nchini Tanzania, Mary O'Neil, aliyefika Ikulu kwa ajili ya kujitambulisha.

Rais Mwinyi alimweleza Balozi huyo kwamba Serikali ya Zanzibar inathamini sana uhusiano na ushirikiano mzuri uliopo kati ya pande hizo na kuishukuru Ireland kuahidi kusaidia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema hatua za Ireland kuahidi kuwawezesha wanawake kutasaidia kwa kiasi kikubwa hasa kwa wanawake wanaojishughulisha na shughuli za kimaendeleo wakiwamo wakulima wa mwani ambao wamekuwa na changamoto ya kukosa soko.

Pia alipongeza hatua ya nchi hiyo kutoa nafasi za masomo nchini humo na kusisitiza haja ya kuendeleza na kuongezwa zaidi hatua hiyo ili Wazanzibari wengi kupata nafasi za masomo mbalimbali nchini humo.

Kuhusu Uchumi wa Bluu, Rais Mwinyi alimweleza Balozi huyo hatua na mikakati iliyowekwa na serikali huku akisema Ireland ina kila sababu za kuunga mkono hatua hizo hasa ikizingatiwa kwamba nchi hiyo imepiga hatua kupitia dira hiyo.

Naye Balozi O'Neil alisena nchi yake itaendelea kuiunga mkono Zanzibar katika kuendeleza sekta mbalimbali za maendeleo ikiwa ni pamoja na kuunga mkono hatua za kuwawezesha wanawake, nafasi za masomo, mazingira ya upatikanaji wa haki kwa jamii, utalii, mabadiliko ya tabia nchi, uchumi wa bluu na sekta nyinginezo.

Katika eneo la utalii, Balozi O'Neil aliahidi atakuwa balozi wa kuitangaza Zanzibar na vivutio vya utalii nchini mwake.

# Wanafunzi 2,600 warejeshwa shuleni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar imewarejesha shuleni wanafunzi 2,609 ambao walitoroka shule kutokana na sababu mbalimbali.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa wizara hiyo, Simai Muhamed Said, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari mjini hapo kuhusu mafanikio ya mwaka mmoja ya wizara hiyo katika kipindi cha uongozi wa Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Alisema wanafunzi hao waliorejeshwa wasichana ni 1,978 na wavulana 631 kutoka Unguja na Pemba. Watoto hao wamerejeshwa shuleni kupitia mradi maalum wa kuwarejesha watoto waliotoroka au ambao hawakuandikishwa kabisa.

Alisema Wilaya ya Micheweni, kisiwani Pemba, inaongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi waliorejeshwa baada ya kutoroka au kutoandikishwa ambao ni 307.

Mbali na kuwarejesha wanafunzi hao, alisema mafanikio mengine yaliyopatikana ndani ya kipindi hiki ni uandikishwaji wa wanafunzi katika ngazi zote za elimu ambao umefikia wanafunzi 552,328 kati ya hao 91,074 ni wa ngazi ya elimu ya maandalizi, 331,425 ngazi ya msingi na 129,829 ngazi ya sekondari.

Simai alisema serikali imeendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaojiunga na elimu ya juu katika vyuo mbalimbali vya ndani na nje ya nchi.

"Idadi ya wanafunzi wanaopatiwa mikopo imeongezeka kutoka wanafunzi 4,040 mwaka 2019/20 hadi wanafunzi 4,316 mwaka 2020/21," alisema Simai.

Waziri huyo alisema pamoja na mafanikio mbalimbali yaliopatikana, bado kuna kazi kubwa ya kufanya hasa ikizingatiwa kuwa matokeo ya wanafunzi katika mitihani yao ya taifa haijawa ya kuridhisha.

Alisema shule bado zinakabiliwa na uhaba wa nafasi hali inayosababisha msongamano mkubwa wa wanafunzi darasani hasa katika ngazi ya elimu ya maandalizi na msingi.

Pia alisema mazingira ya kujisomea bado yanahitaji kuimarishwa kwa sababu shule nyingi hazina vyoo vya kutosha na wanafunzi wengi wa ngazi ya elimu ya msingi na maandalizi wanakaa sakafuni.

Alisema wizara yake imejipanga kuzipatia changamoto zote hizo utatuzi wa kudumu na mwaka wa pili wa uongozi wa Dk. Mwinyi, zimetenga Sh. bilioni 69 kwa ajili ya kuimarisha sekta ya elimu.

Alisema fedha hizo zinatokana na mkopo wa Sh. bilioni 230 kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) kwa ajili ya mapambano dhidi ya janga la corona.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi akifurahia jambo wakati akizungumza na mgeni wake Muigizaji maarufu wa sinema kutoka nchini India, Sanjay Dutt, Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Waziri abainisha uwezo wanawake katika kuleta mabadiliko ya jamii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Saada Mkuya, amesema wanawake wana uwezo wa kupambania maendeleo kupitia nyanja mbalimbali.

Mkuya aliyasema hayo katika hafla ya uzinduzi wa kitabu kilichoandikwa na mwandishi wa habari mkongwe, Zuhra Yunus, uliofanyika mjini hapo.

Akizungumzia kitabu hicho, alisema amefurahishwa na maudhui yaliyomo kwa kuwa kinafundisha mambo mengi na kinaonyesha jinsi mwanamke anavyoweza kuleta mabadiliko kwenye jamii.

Waziri alimpongeza mwandishi kwa jitihada zake ambazo alisema zimeinua hadhi ya mwanamke wa Kizanzibari na kuiongezea thamani historia ya visiwa hivyo kwa kuonyesha ukweli uliokosa sauti.

"Hii simulizi ya mwanamke aliyesimamia kile alichokiamini, iwe chachu ya kuamsha ari kwa wengine kufanya utafiti na kuandika vitabu vingi zaidi kuhusu utajiri mkubwa wa historia na maudhui mengine kuhusu Zanzibar ambayo vinaweza kutumika kufundishia katika shule zetu," alisema Waziri Mkuya.

Alisema kitabu hicho kinaonyesha pia umuhimu wa elimu kwa wanawake wa Kizanzibari na nguvu walizo nazo iwapo wanapewa nafasi.

Naye Mwandishi Zuhra alisema kitabu hicho alianza kukusanya maudhui yake tangu mwaka 2017.

Alisema licha ya wanawake kushiriki kupigania Mapinduzi ya Zanzibar, wamesahaulika kutajwa kwenye historia na badala yake kuonekana jambo hilo lilifanywa na wanaume peke yao.

Zuhra alimtaja mmoja wa wanawake walioshiriki mapinduzi hayo ni Biubwa Amour Zahor, ambaye amemfichua baada ya kumwandikia kitabu kuhusu historia yake na ushiriki wake katika harakati za Mapinduzi ya Zanzibar kinachoitwa 'Biubwa Amour Zahor Mwanamke Mwanamapinduzi'.

Alisema kilichomsukuma kuandika kitabu hicho ni kuwatambua wanawake Wazanzibari ambao walijitoa na kuwa sehemu ya mapinduzi lakini wamesahaulika.

Kitabu hicho chenye kurasa 220, kinaelezea changamoto na jinsi mwanamapinduzi huyo, Biubwa, alivyojitosa kuhakikisha ukombozi wa taifa unapatikana huku akipitia changamoto mbalimbali na kunusurika kubakwa.

Alisema ushiriki wa Biubwa katika mapinduzi haukuwa katika kujipatia cheo wala sifa bali kutoa mchango wake muhimu katika kuwezesha mapinduzi jambo ambalo ni nadra katika siasa.

Kitabu hicho, alisema kinaeleza mwanamke huyo alivyokuwa bega kwa bega na wanaume katika kupigania uhuru wa kweli na kupigania nchi yake.

Akizungumza wakati wa kuzindua kitabu hicho mwanaharakati wa haki za wanawake, Salma Maulid, alisema kitabu hicho kitafumbua macho watu wengi katika harakati za mwanamke na mitazamo kuhusu ushiriki wa wanawake katika harakati za ukombozi wa mataifa yao.

"Yaliyomo kwenye kitabu hiki ni taswira kwamba wanawake wana mchango mkubwa na wanaweza kufanya mambo makubwa, lakini hayasemwi wala hayaandikwi yakafahamika," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

GARI INAUZWA AINA YA VOLKSWAGEN TOUREG YA MWAKA 2004 NAMBA DDV RANGI NYEUSI. INATEMBEA NA IKO KWENYE HALI NZURI SANA. BEI NI TSH. 15,000,000/- PIGA SIMU NAMBA 0762 810 451.

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**GALLIS R MAKUNJA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0316/0220 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya KIBASILA mwaka 2014,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa DAR/MAG/R-B/532658/2021


## KUPOTEA KWA CHETI



**GLORIA PONSIAN BAYONA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S2499-0784** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia TUSIIME SEKONDARI mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **WIMB/RB/418/2021.**

116561902

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**KELVIN SYLVESTER IHUYA** anatangaza kupotelewa na result slip ya kidato cha sita yenye index namba **S1599/0520** iliyotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya **secondary BAOBAB** mwaka 2021, yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **KW/RB/5432/2021**

116562102

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA TARIME**
**RUFAA NA. 88 YA 2021**
**GHATI EFRAIM……………………………MRUFANI**
**DHIDI YA**
**ANASTAZIA PROSPA……………………………MRUFANIWA**

**Mrufaniwa ANASTAZIA PROSPA popote ulipo.**

Fahamu kwamba mrufani GHATI EFRAIM ameleta Rufaa Na. 88/2021, dhidi yako.
Hivyo basi kama unakusudia kupinga rufaa hiyo unatakiwa kuleta majibu yako na uwepo barazani wewe binafsi, wakili wako au mwakilishi anayekubalika kisheria, tarehe 3/12/2021, siku ambayo shauri limepangwa kutajwa.

Endapo hutatekeleza hayo, shauri litaendelea upande mmoja dhidi yako na maamuzi kutolewa.

Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 28/10/2021.

NGUKULIKE, N.O
MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) TARIME.

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO**
**SHERIA YA UMILIKISHAJI WA ARDHI YA MWAKA 1999**
**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI**
**BARUA YA TOLEO YENYE KUMB.NA. MG/LD/13358/1**
**MMILIKI ALIOANDIKISHWA: MARY FLORENCE ASSEY**
**S.L.P 20, MOROGORO.**
**ARDHI: KIWANJA NA 413 KITALU "D" TUNGI MANISPAA YA MOROGORO**
**MUOMBAJI: MARY PHILIPO ASSEY**
**S.L.P 20, MOROGORO.**

Taarifa inatolewa kwamba **BARUA YA KUMILIKI ARDHI** iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa **NAKALA HALISI YA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iwapo hakuna pingamizi litakalo tolewa kwa muda wa mwezi mmoja toka tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti.
**HATI YA BARUA HALISI YA TOLEO** ikionekana, irudishwe kwa **MKURUGENZI WA MANISPAA-MOROGORO S.L.P 166 MOROGORO**

Valency HK
KNY: MKURUGENZI WA MANISPAA MOROGORO

**IN THE DISTRICT COURT OF MULEBA AT MULEBA.**
**CASE NO…32…….. 2021**
**ERADSON NICOLAUS.**
**APPEALLANT/APPLICANT**
**VS**
**HALIMA IDRISA. RESPONDENT**
**NOTICE OF DATE MENTION/ HEARING.**

**TAKE NOTICE** that above case has been fixed for Mention / Hearing on 17th day of November 2021 at 8:00 am.
Before **Hon A.H.MWETINDWA SRM.**
YOU ARE. Required to appear before this Court within fail and you must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.
Given under my Hand the seal of the Court this 4th day of November 2021.

……………………………………
RESIDENT MAGISTRATE
COPY TO BE SERVED UPON.
HALIMA IDRISA
OF KISANA VILLAGE
C/O WEO KYEBITEMBE.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SOPHIA HALFAN SWAI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 309 DFF – LANDCRUISER.** Chassis namba **URJ2024095497.** Engine namba **1UR0516527.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PWA/MAP/RB/521229/2021.**

116562002

**IN THE DISTRICT COURT OF MULEBA AT MULEBA.**

**CASE NO…31…….. 2021**
**NICOLAUS BAGANTEGA.**
**APPEALLANT/APPLICANT**
**VS**
**HALIMA IDRISA. RESPONDENT**
**NOTICE DATE MENTION/ HEARING.**

**TAKE NOTICE** that above case has been fixed for Mention / Hearing on 17th day of November 2021 at 8:00 am.
Before Hon A.H.MWETINDWA SRM.
YOU ARE. Required to appear before this Court within fail and you must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.
Given under my Hand the seal of the Court this 4th day of November 2021.

……………………………………
RESIDENT MAGISTRATE
COPY TO BE SERVED UPON.
HALIMA IDRISA
OF KISANA VILLAGE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Mahakama ya Mwanzo MAKOLE**
**Wilaya ya DODOMA**

**MADAI NAMBARI 149/2021**

**MDAI……………………………CPT RAPHAEL MARWA**

**DHIDI YA**

**MDAIWA……………………………RAJABU MAJIGE**

**KWA: RAJABU MAJIGE**

**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba MADAI YA PESA TSH.2,354,000/=**

Kwa hiyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya ALHAMIS tarehe 18/11/2021 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujijitetea katika shauri hilo.
Angalia kama *hukuhudhiria siku ilitajwa hapo juu. Mahakama ikithibitisha kama *umepokea kuitwa kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 09/11/2021

Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo.

1116562802

**FORM 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 129 OF 2021**

**In the Matter of the Estate of the Late SIHOFU LINDA GEORGE MALLYA**

**and**

**In the Matter of Application for letters of administration by ELIMARY LINDA MALLYA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner. Objections to the grant should be filed on or before the 25th day of November, 2021.
Dated at Dar es salaam this 8th day of November, 2021.

Registrar/Senior Resident Magistrate

1116562902

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AHMED ALLY HEMED** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 168 BKA – SCANIA 124.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/STA/RB/533387/2021.**

116563002

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## WFP kutoa chakula Zimbabwe

**New York, MAREKANI**

SHIRIKA la Chakula Duniani (WFP), limesema tathmini inaonyesha kwamba zaidi ya watu milioni tano katika taifa hilo la Kusini mwa Afrika, wanatarajia kushuhudia uhaba wa chakula katika miezi ijayo.

Belinda Popovska, msemaji wa WFP, Zimbabwe, ameiambia VOA kwamba shirika hilo limeanza kuangalia kupata ufadhili kwa ajili ya kuagiza chakula kwa wale wanaohitaji.

Belinda alisema ripoti za karibuni za mwaka huu katika maeneo ya vijijini Zimbabwe, iliyotolewa na kamati ya tathmini imeashiria kwamba kiasi cha watu milioni 2.9 ambao ni sawa na asilimia 27 ya kaya wataendelea kukumbwa na ukosefu wa chakula wakati wa kipindi cha baada ya mavuno, Januari na Machi mwaka 2022.

Katika maeneo ya mijini, hadi watu milioni 2.4 walitarajiwa kutokuwa na chakula cha kutosha kwa mujibu wa tathmini iliyofanywa karibuni kwenye maeneo ya mijini mwaka huu wa 2021.

Serikali ilisema Zimbabwe mwaka huu imepata mavuno mengi, ukosefu wa chakula katika maeneo ya vijijini unaashiria kuwa mavuno kwa hakika hayakuwa makubwa hivyo.

Waziri wa Habari Monica Mutsvangwa, alisema uhaba wa chakula utamalizika kukiwa na uzalishaji zaidi mashambani katika msimu ujao wa mwaka 2021/2022 ambao unatarajiwa kuanza wakati wowote kuanzia sasa.

Aliongeza kusema kwamba serikali itahakikisha kuwa wakulima wana bidhaa za kutosha na fedha wanazohitaji ili kukidhi mahitaji ya wote, binadamu na matumizi ya viwandani.

Zimbabwe, iliwahi kuwa mzalishaji mkubwa wa chakula katika eneo hilo kwa miaka mingi imekabiliwa na uhaba wa chakula na kulazimishwa kutegemea misaada ya taasisi za kibinadamu kama World Vision, USAID na WFP ili kuwalisha watu wake.

Serikali inalaumu matatizo ya kutokea ukame wa mara kwa mara, wakosoaji wake wanazungumzia program ya mageuzi ya ardhi, iliyokuwa na ovyo, ambayo ilianza mwaka 2000 na kuwakosesha makazi wakulima wa kizungu kutoka kwenye ardhi zao.

**VOA**

**Waziri wa Habari Monica Mutsvangwa, alisema uhaba wa chakula utamalizika kukiwa na uzalishaji zaidi mashambani katika msimu ujao wa mwaka 2021/2022 ambao unatarajiwa kuanza wakati wowote kuanzia sasa.**

# Rwanda yakana kujihusisha na mashambulizi ya M23

**Kigali, RWANDA**

JESHI la Ulinzi la Rwanda, limesema halihusiki wala kuunga mkono kundi la zamani la M-23.

Imeripotiwa kuwa kundi la watu wenye silaha linaloaminika kuwa waasi wa M-23, mwishoni mwa wiki walivuka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kutoka Uganda, yaliko makazi yao kushambulia na kudhibiti Tshanzu na Runyoni.

Waasi wa zamani wa M23, wanaoelezwa hawakuomba hifadhi ya ukimbizi Rwanda wakati walipoondolewa DRC mwaka 2013, wamekuwa nchini Uganda, ambako ndiko shambulizi lilikoanzia na ambako kundi hilo lenye silaha lilipoondoshwa.

Jeshi la nchi hiyo lilisema taarifa zozote zinazodai kuwa kundi hilo lilianzia Rwanda ni propaganda za kudhoofisha mahusiano mazuri kati ya Rwanda na DRC.

**BBC**



Wahamiaji katika msafara wakielekea eneo la Arriaga, nchini Mexico, juzi. Maelfu ya wahamiaji wamekuwa wakiingia kwenye nchi hiyo kutokea nchi jirani ili kuomba makazi. **PICHA REUTERS**

## Rais Chakwera ataka raia waache kuwaomba wanasiasa

**Lilongwe, MALAWI**

RAIS wa Malawi, Lazarus Chakwera, amewataka raia kila mmoja kuwajibika katika kuleta maendeleo ya nchi hiyo badala ya kuyadai kutoka kwa wanasiasa.

Alisema alikuwa na nia ya ujumbe kwenye simu yake watu wakimtaka kuziendesha familia zao kwa sababu tu yeye ni rais, akiongeza kuwa wabunge walipata ujumbe wa namna hiyo kutoka kwenye majimbo yao. "Lazima tujitibu tabia ya kuomba kwa wanasiasa kuliko tunachokitaka kutoka kwetu wenyewe...nchi yetu haitaendelea kwa tabia ya namna hii," alisema.

Rais huyo aliwataka raia kutekeleza mipango katika ngazi ya familia ambayo inakwenda sambamba na mpango wa maendeleo wa taifa ambao alikua akiuzindua.

Alitoa mfano mpango wa kuimarisha uzalishaji, kilimo cha biashara ambao amesema hautafanikiwa kama hakutakuwa na mabadiliko katika ngazi ya familia.

**BBC**

# UN: Ethiopia hatarini vita wenyewe kwa wenyewe

**Addis Ababa, ETHIOPIA**

UMOJA wa Mataifa (UN), umeonya kuwa Ethiopia iko katika hatari ya kutumbukia katika vita vya wenyewe kwa wenyewe, vinavyoongezeka ikiwa mapigano katika eneo la Kaskazini la Tigray, hayatakoma.

Mkuu wa Masuala ya Kisiasa na Ujenzi wa Amani wa Umoja wa Mataifa, Rosemary DiCarlo, alisema hakuna malori ya misaada yaliyofika mji mkuu wa Tigray, Mekelle tangu katikati ya Oktoba, licha ya watu milioni saba kuhitaji msaada wa haraka wa chakula.

UN, ilisema watu 400,000 kati ya wale wenye uhitaji wanaishi katika hali ya njaa.

Akihutubia baraza hilo, mjumbe wa Umoja wa Afrika (AU) katika Pembe ya Afrika, Olusegun Obasanjo, alisema amekutana na Waziri Mkuu Abiy Ahmed na kiongozi wa eneo la Tigray, Debretsion Gebremichael.

Alisema wote wawili walikubaliana kuwa mzozo huo ulikuwa wa kisiasa, ingawa hakuna mazungumzo ya moja kwa moja kati ya pande hizo mbili.

Baraza la Usalama linataka wanajeshi na wanamgambo kuondoka katika eneo hilo, ili kuwezesha upatikanaji wa chakula na dawa zinazohitajika sana.

Msemaji wa Waasi wa Tigray alisema vikosi vyao vitaendelea kusonga mbele hadi mji mkuu wa Ethiopia, Addis Ababa, hadi serikali iondoe vikwazo vyake katika eneo la Kaskazini.

Getachew Reda alikiambia kipindi cha redio cha BBC Focus on Africa kwamba, kikwazo pekee ambacho kilikuwa kikizuia njia ya amani ya Ethiopia ni "takwa la Waziri Mkuu Abiy Ahmed na suluhisho la kijeshi kwa kile ambacho kimsingi ni shida ya kisiasa".

Waasi wanasonga mbele kuelekea mji mkuu na serikali imewataka wakazi wa Addis Ababa, kuhamasisha na kulinda vitongoji vyao.

**BBC**

# SERIKALI BEGA KWA BEGA NA STARS KUIFURUSHA DR CONGO

**Na Saada Akida**

WAKATI Taifa Stars ikishuka Uwanja wa Benjamin Mkapa kesho kuikaribisha DR Congo kwenye mechi ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia Qatar 2022, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbas, amesema serikali imejipanga vizuri kuhakikisha wanasimamia kikamilifu timu za taifa, ikiwamo ya watu wenye ulemavu, 'Tembo Warriors' inayojiandaa na michuano ya Afrika.

Baada ya mechi hiyo, Taifa Stars itaifuata Madagascar katika mechi ya mwisho ya hatua hii ya makundi, wakati Tembo Warriors yenyewe itakuwa mwenyeji wa michuano hiyo inayotarajiwa kuanza Novemba 25, mwaka huu hapa nchini.

Taifa Stars wanaongoza Kundi J, wakiwa na pointi saba sawa na Benin ambayo inayoshika nafasi ya pili kutokana na kuzidiwa kwa idadi ya mabao ya kufunga, wakati DR Congo wakiwa nafasi ya tatu kwa alama tano na Madagascar wakiburuza mkia kwa pointi tatu.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Dk. Abbas alisema serikali inaendelea kusimama kidete kuhakikisha Taifa Stars inafanya vizuri katika michezo yote miwili, dhidi ya DR Congo ambao watacheza nao kesho, ukiwa ni mchezo muhimu kupata matokeo chanya.

Alisema kuelekea mchezo huo, leo Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa, atatembelea kambi ya Stars kwa ajili ya kutia hamasa na motisha kwa wachezaji wa timu hiyo.

"Kuelekea mchezo huu wa Alhamisi (kesho), serikali haina tashititi wala jaka la moyo, tumefanya maandalizi mazuri ikiwamo kupata nafasi ya mashabiki 30,000 kuingia uwanjani kushuhudia na kusapoti timu yetu ya taifa katika mchezo muhimu wa kuwania nafasi za timu 10 ambazo zitawania kufuzu kucheza Kombe la Dunia.

"Tunahamasisha Watanzania kujitokeza kuisapoti timu yao, shabiki ni mchezaji wa 12, ambaye atakuja kuwatia moyo wachezaji wetu, kwani kushirikishi michuano hii ni tukio kubwa sana na fahari kwa nchini yetu hasa kwa hatua hii tuliyofikia," alisema Dk. Abbasi.

Alisema tayari serikali imeshaandaa ndege kubwa kwa ajili ya wachezaji kwenda nchini Madagascar na kurudi baada ya mechi ya nwisho ya makundi dhidi ya wenyeji hao.

Aidha, Dk. Abbas aliwataka Watanzania kuanzia leo kuanza hamasa 'vaibu' kila kona ikiwamo katika mitandao ya kijamii huku daladala na bodaboda akitaka kuning'iniza bendera ya Tanzania kwa ishara ya hamasa kuelekea mchezo huo.

Mbali na Stars, Dk. Abbas alisema serikali imetoa kiasi cha Sh. milioni 135 kusaidia mashindano makubwa ya Afrika ya mpira wa miguu kwa watu wenye ulemavu ambayo Tanzania ni wenyeji wa michuano hiyo itakayotoa timu nane kwenda kucheza Kombe la Dunia kwa walemavu.

"Tanzania tunawakilishwa na Tembo Warriors, huu ujio wa mashindano hayo ikiwa ni wenyeji, ni ishara kubwa sana na dalili nzuri kwa taifa letu," alisema.

Naye Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wilfred Kidao, alisema kwa upande wa maandalizi ya Stars yanaendelea vizuri na kuishukuru serikali kwa kutimiza vigezo vya Covid -19 na kuruhusiwa mashabiki 30,000.

"Mashabiki wajitokeze kwa wingi na TFF tumeweka viingilio rahisi kwa VIP B na C ni Sh. 5,000 huku mzunguko ikiwa ni Sh. 3,000. Tumeweka bei rahisi ili kuwapa nafasi Watanzania kuingia kwa wingi kuisapoti timu yao," alisema Kidao.

Naye mdau wa soka nchini, Azim Dewji, ametoa jezi 2,000 kwa wanafunzi ambao watajitokeza kuisapoti Stars na kuwataka mashabiki wa soka kuungana kuwa pamoja na kuziweka pembeni tofauti zao za U-Simba na U-Yanga.

"Alhamisi tunatambua ni siku ya kazi, basi tunaomba serikali itoe nusu siku kwa watu kukaa ofisini na kuwapo kwa mapumziko ili kuwapa nafasi Watanzania kwenda uwanjani kutoa sapoti.

"Binafsi nimenunua tiketi 100 kwa wafanyakazi wangu na kuwapa nusu siku kufanya kazi baada ya hapo kila mmoja tunaongozana kuja uwanjani kuisapoti Stars, hii iwe mfano kwa kampuni na hata ofisi za serikali," alisema Azim.

**WAPELEKEE...**



Mdau wa michezo nchini, Azim Dewji (katikati), akimkabidhi jezi Kaimu Katibu Mkuu Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Neema Msita, kwa niaba ya wanafunzi wa shule mbalimbali kwa ajili ya kuzivaa kesho watakapokwenda Uwanja wa Benjamin Mkapa kuishangilia timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, wakati mechi dhidi ya DR Congo, kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika mwakani nchini Qatar. Kulia ni Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbas. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mary G, Barnaba Classic waachia 'I Feel You'

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

MWANAMUZIKI anayechipukia katika medani ya muziki wa Bongo Fleva, Mary Godfrey 'Mary G', ameachia kibao kikali kinachokwenda kwa jina la "I Feel You".

Akizungumza na Nipashe jana, mwanamuziki huyo ambaye ni mwanafunzi wa mwaka wa tatu katika Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino (SAUTI), akichukua shahada ya sheria, alisema kibao hicho, amemshirikisha msanii mkongwe, Barnaba Classic.

"Huu wimbo nimemshirikisha Msanii wa Bongo Fleva, Barnaba Classic, unaitwa 'I Feel You'", alisema Mary G.

Msanii huyo alisema aliamua kumshirikisha Barnaba kwa kuwa anaamini msanii huyo ana kipaji na yuko vizuri katika uimbaji.

Alisema Barnaba ni miongoni mwa wasanii wanaofanya vizuri hapa nchini, hivyo anaamini kwa kumshirikisha katika ngoma hiyo wimbo huo utakuwa juu.



Aidha, Mary G alisema wimbo huo umetanguliwa na nyimbo nyingine nne ambazo ni 'Take Over, Nipotezee, Turning Back na Promise'.

Msanii huyo alisema licha ya kuwa amebanwa na masomo, lakini anatarajia kumaliza kurekodi albamu yake ya kwanza hivi karibuni na kwamba katika nyimbo zijazo ana mpango wa kuwashirikisha wasanii nguli nchi wa Bongo Fleva.

"Kuna wasanii nawakubali sana katika Bongo Fleva ambao ni Nassib Abdul 'Diamond Platinum' na Ali Kiba 'King Kiba' kwa kweli wako vizuri katika muziki," alisema.

## Mangungu awatoa hofu mashabiki Simba

**Na Adam Fungamwango**

MWENYEKITI wa Klabu ya Simba, Murtaza Mangungu, amewatoa hofu wanachama na mashabiki wa Simba, akiwataka kuwaacha viongozi kufanya mabadiliko na kutekeleza majukumu ambayo wamewapa kwa niaba yao, huku akitanabaisha kuwa Kocha Mkuu, Pablo Franco Martin, atawasili wiki hii.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mangungu alisema mpaka sasa bado wanaendelea na mchakato wa kupata kocha wa viungo na makipa, na kocha atakayekuja ataendelea kuwa na makocha waliopo Thierry Hitimana na Selemani Matola hadi hapo kutakapokuwa na mabadiliko mengine.

"Timu iko vizuri na tunategemea kufanya vizuri, Kocha Mkuu atawasili wiki hii na atakuwa akifundisha na makocha waliopo hadi hapo kutakapokuwa na mabadiliko mengine. Tunandelea na mchakato wa makocha wa viungo na makipa, hivyo wanachama na mashabiki wa Simba ambao wametupa dhamana ya kuongoza naamini wana utulivu, na nawataka waondoe hofu, wakati huu tunaendelea kufanya mabadiliko ambayo tunayaona ni lazima tuyafanye kwa wakati huu," alisema Mangungu.

## Kocha wa Zimamoto ataja sababu sare

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

HUKU kikosi chake kikiwa kimeshinda mchezo mmoja tu kati ya mitatu ya Ligi Kuu Zanzibar, Kocha Mkuu wa Zimamoto FC, Mohamed Ali Hilali 'Tedy', amesema tayari amebaini tatizo linalowafanya kukosa ushindi.

Zimamoto ambayo imeshuka dimbani mara tatu imetoka sare michezo miwili na kushinda mmoja katika dimba la Gombani Kisiwani Pemba.

Akizungumza na gazeti hili jana, Tedy alisema katika michezo mitatu yote ameona mapungufu madogo ambayo ni kawaida katika soka, yaliyosababisha kupoteza nafasi nyingi katika michezo miwili waliyotoka sare.

Alisema miongoni mwa mapungufu hayo ni wachezaji kupoteza umakini, kutofanya maamuzi ya haraka pale wanapokuwa na mpira au hata mpira unapokuwa miguuni mwa wapinzani wao.

Alisema kukosa mbinu za kiuchezaji pamoja na ujanja ndicho kinachosababisha wachezaji wake kutokuwa na ubunifu pale wanapopata mipira au hata kunyang'anya mipira, jambo ambalo sasa anakwenda kulifanyia kazi.

## ZISIKUPITE

### SOLSKJAER KUBAKI UNITED
OLE Gunnar Solskjaer anatarajia kuendelea kuwa Kocha wa Manchester United kwa mechi ijayo dhidi ya Watford baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa. **(Guardian)**

### JONES AGOMBEWA EPL
KLABU ya Watford na Newcastle zinamwania mlinzi wa Manchester United na England, Phil Jones mwenye umri wa miaka 29 kwa mkopo. **(Sun)**

### OVERMARS AIKATAA NEWCASTLE
MKURUGENZI wa Soka wa Ajax, Marc Overmars, amekataa nafasi ya kujiunga na Newcastle United. **(Athletic)**

### GERRARD NAMBA MOJA VILLA
KLABU ya Aston Villa imemfanya kocha wa Rangers, Steven Gerrard kama chaguo lao la kwanza kumrithi Dean Smith, huku pia kocha wa Ubelgiji, Roberto Martinez akihusishwa na nafasi hiyo. **(Sun)**

### RIO ATAKA OLE ATIMULIWE
RIO Ferdinand, mshindi mara sita wa Ligi Kuu England akiwa na Manchester United, ameishauri klabu hiyo kumfukuza kocha Ole Gunnar Solskjaer baada ya kuwa na matokeo mabaya. **(YouTube, via Mirror)**

### LAMPARD ANUKIA NORWICH
KOCHA wa zamani wa Chelsea, Frank Lampard yupo kwenye rada za kuwaniwa kupewa nafasi kule Norwich City pamoja na kocha wa Southampton, Ralph Hasenhuttl. **(Sky Sports)**

### RAMSEY KUACHIWA JUVE
JUVENTUS itakuwa tayari kumwachia kiungo wa kimataifa wa Wales, Aaron Ramsey kama mchezaji huru Januari licha ya kubakiwa na miezi 18 kwenye mkataba wake wa sasa. **(Calciomercato)**

### SPURS KUMSAJILI VLAHOVIC
TOTTENHAM Hotspur itailipa Fiorentina pauni milioni 60 na kuwapiku wapinzani wao wa Jiji la London, Arsenal kwenye mbio za kuwania kumsajili mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Serbia, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 21. **(La Nazione, via Express)**

### NIGUEZ KUBAKI CHELSEA
KIUNGO wa Hispania, Saul Niguez mwenye umri wa miaka 26, anajiandaa kubaki Chelsea kwa mkopo wa muda mrefu akitokea Atletico Madrid, licha ya kucheza dakika mbili tu kwenye Ligi Kuu England tangu atue hapo Agosti, mwaka huu. **(Telegraph)**

### MAITLAND-NILES ANOGEWA ARSENAL
KIUNGO wa Arsenal na England, Ainsley Maitland-Niles mwenye umri wa miaka 24, amesema ana furaha kubakia kwenye klabu hiyo, baada ya kujaribu kuondoka wakati wa dirisha la majira ya joto. **(PA Media, via Mail)**

### STRAKOSHA ATAKIWA NEWCASTLE
KLABU ya Newcastle United inataka kumsajili golikipa wa Lazio na Albania, Thomas Strakosha mwenye umri wa miaka 26 wakati wa dirisha la Januari. **(Sun)**

### WOODWARD KUENDELEA UNITED
ED Woodward yupo kwenye mazungumzo ya kuchukua nafasi ya mshauri wa Manchester United wakati atakapostaafu nafasi ya makamu mwenyekiti mtendaji mwezi ujao. **(Mail)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# POGBA AONDOLEWA KIKOSI CHA UFARANSA

●●●Sasa kuikosa Kazakhstan Jumamosi na Finland Novemba 16, mechi za kuwania kufuzu Kombe la Dunia...

**PARIS, Ufaransa**

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba, ameondolewa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Ufaransa kinachojiandaa na mechi za kufuzu Kombe la Dunia mwakani, kutokana na kuumia nyama za paja.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia mwenye umri wa miaka 28, aliumia kwenye mazoezi Jumatatu, Shirikisho la Soka la Ufaransa (FFF), limethibitisha.

Pogba hatakuwapo kwenye mchezo wa Jumamosi dhidi ya Kazakhstan na ule dhidi ya Finland, Novemba 16.

Tayari alikuwa anaukosa mchezo wa United ujao dhidi ya Watford kwenye Ligi Kuu ya England, Novemba 20, mwaka huu, wakati akitumikia adhabu ya kufungiwa mechi tatu.

Pogba alilimwa kadi nyekundu wakati wa mchezo wa nyumbani wakichezea kichapo cha mabao 5-0 kutoka Liverpool, Oktoba 24.

FFF ilisema Pogba "ameumia kwenye paja la mguu wa kulia".

Ufaransa inahitaji ushindi mmoja tu ili iweze kufuzu michuano ya Kombe la Dunia Qatar 2022.

Kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer, tayari anawakosa wachezaji kadhaa kutokana na kuwa majeruhi.

MECHI KALI
HOME
AWAY
KOSOVO
1.94 | 3.55 | 3.80
JORDAN

CHEZA USHINDE
JACKPOT
TZS. 667

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# HOWE KOCHA MPYA NEWCASTLE

**NEWCASTLE, England**

KLABU ya Newcastle United imemteua, Eddie Howe kuwa kocha wake mkuu wakati wakipambana kuhakikisha wanabaki Ligi Kuu England.

Howe mwenye umri wa miaka 43, amekuwa hana kazi tangu alipoondoka Bournemouth Agosti 2020 baada ya kushindwa kuwanusuru kushuka daraja.

Hakuwa chaguo la kwanza kwa matajiri wapya wa klabu hiyo, kwani kocha wa Villarreal, Unai Emery, ndiye alikuwa akipewa nafasi kubwa kabla ya kuikataa ofa hiyo.

Lakini Howe anachukuliwa kama mmoja wa makocha bora vijana kwenye soka la Uingereza na sasa atakuwa na nafasi ya kuijenga upya Newcastle.

Baada ya kuteuliwa, Howe alisema: "Ni heshima kubwa kuwa kocha mkuu wa klabu hii na historia ya Newcastle. Ni fahari kubwa kwangu mimi na familia yangu.

"Hii ni nafasi ya aina yake, lakini pia kuna kazi kubwa ya kufanya mbele ya safari na naamini kwamba, nina kazi kubwa ya kufanya.

"Ningependa kuwashukuru wamiliki wa klabu hii na ninaamini nitakuwa na nafasi nzuri ya kufanya makubwa hapa."

# De Jong kubadilishwa na Sterling



**MANCHESTER, England**

MIAMBA ya soka ya Ligi Kuu England, Manchester City inaweza kuwasilisha ofa ya kubadilishana wachezaji na Barcelona ikiwahusisha Frenkie de Jong na Raheem Sterling.

Barcelona wamehusishwa sana na nia ya kumnunua mchezaji wa kimataifa wa England, Sterling mwaka 2022 baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, kuonekana kutokuwa kipaumbele kwenye mipango ya kocha Pep Guardiola.

Guardiola amekiri kuwa hataweza kumzuia Sterling kama angetaka kuondoka ili kupata muda zaidi wa kucheza licha ya kwamba bado ana umuhimu kwenye kikosi cha City.

Kwa mujibu wa ripoti kutoka El Nacional, kocha mpya wa Barcelona, Xavi anataka kuleta wachezaji wapya na Guardiola anaweza kujaribu kuwasilisha ofa ya kubadilishana kwa de Jong.

Guardiola ni shabiki wa muda mrefu wa nyota huyo wa Uholanzi, tangu enzi zake akiwa na Ajax, lakini anakabiliwa na changamoto ya namna ya kumwondoa Barcelona kwa sasa.

Ripoti zinasema Xavi hajalipa kipaumbele suala la kuuzwa kwa De Jong, lakini nafasi ya kumsajili Sterling inaweza kubadilisha mawazo yake, na Barcelona wanaweza kukubali ada ya euro milioni 20 pamoja na winga huyo wa zamani wa Liverpool.

7,771,400

JACKPOT
MECHI WIKI HII

# SMITH ROWE AITWA KWA MARA YA KWANZA ENGLAND



**LONDON, England**

NYOTA wa Arsenal, Emile Smith Rowe, ameitwa kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya England kwa mara ya kwanza.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 21, ameungana na kikosi cha England kinachofanya mazoezi pale St. George's Park Jumatatu, katika maandalizi ya kuelekea jukumu la kimataifa la kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Albania na San Marino.

Marcus Rashford, James Ward-Prowse, Mason Mount na Luke Shaw wameshindwa kuungana na kikosi hicho kwa sababu ya changamoto za majeraha.

Rowe, aliyetarajiwa kuungana na kikosi cha vijana chini ya umri wa miaka 21, ameungana rasmi na wenzake kutimiza ndoto yake ya kuchezea timu ya taifa, ambayo ni ndoto ya kila mchezaji anayecheza soka la kulipwa.

Rowe amecheza mechi zote za Arsenal msimu huu na amecheka na nyavu katika kila mchezo kwenye mitatu ya ligi ya mwisho.

Kuchaguliwa kwake ni zawadi ya kufanya vizuri kwenye ligi akiwa na Arsenal na ambayo hivi sasa imekuwa na matokeo mazuri.


# Laporta: Haikuwa rahisi kumpata Xavi

**BARCELONA, Hispania**

RAIS wa Klabu ya Barcelona, Joan Laporta, ameweka wazi kuwa haikuwa kazi rahisi kukamilisha uhamisho wa kocha wao mpya, Xavi Hernandez kutoka klabu ya Al Sadd hasa kwenye kipindi hichi cha ukata wanachopitia.

Laporta hakusafiri kwenda jijini Doha kufanya makubaliano na klabu ya Al Sadd katika uhamisho wa Xavi badala yake aliwatuma makamu wake, Mateu Alemany na Rafa Yuste kufanikisha uhamisho huo.

Uhamisho huo umechukua muda kukamilikia kutokana na ukata ambao



klabu ya Barcelona inapitia.

Xavi mwenyewe alilazimika kutoa kiasi fulani cha fedha ili kukamilisha uhamisho huo, Barcelona haikuweza kufanikiwa kuvunja mkataba ambao ulikuwa na thamani ya euro milioni 5.

Laporta hakuweza kutoa maelezo kwenye utambulisho wa xavi, "kufanikisha kuondoka Al Sadd, klabu na Xavi walishirikiana kuwa kitu kimoja na tumefanikiwa, haya ni maelezo kwa kifupi," alisema Laporta.

Xavi sasa ni kocha rasmi wa klabu ya Barcelona na ameshapewa mikoba ya kuiondoa nafasi ya tisa kurudi kwenye ushindani wake na kuhakikisha kuwa anaivusha kwenye Ligi ya Mabingwa barani Ulaya.

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 13/11/21 | 18:00 | Rochdale vs Leyton Orient | 2.27 | 3.28 | 2.99 |
| 02. 13/11/21 | 18:00 | Tranmere vs Sutton United | 2.32 | 3.23 | 2.94 |
| 03. 13/11/21 | 18:00 | Stevenage vs Mansfield | 2.46 | 3.20 | 2.76 |
| 04. 13/11/21 | 18:00 | Bristol Rovers vs Northampton | 2.41 | 3.19 | 2.85 |
| 05. 13/11/21 | 18:00 | Walsall vs Harrogate | 2.60 | 3.23 | 2.60 |
| 06. 13/11/21 | 18:00 | Altrincham vs Boreham Wood | 2.83 | 3.27 | 2.35 |
| 07. 13/11/21 | 18:00 | Yeovil vs Eastleigh | 2.38 | 3.22 | 2.83 |
| 08. 13/11/21 | 18:00 | Wealdstone vs Barnet | 2.43 | 3.41 | 2.63 |
| 09. 13/11/21 | 18:00 | Accrington vs Plymouth | 2.70 | 3.44 | 2.39 |
| 10. 13/11/21 | 20:15 | Mirandes vs Huesca | 2.34 | 3.14 | 2.99 |
| 11. 14/11/21 | 18:00 | UD Ibiza Eivissa vs Almeria | 3.13 | 3.18 | 2.24 |
| 12. 14/11/21 | 20:15 | Leganes vs Real Oviedo | 2.29 | 2.99 | 3.23 |
| 13. 14/11/21 | 20:15 | Burgos vs Ponferradina | 2.41 | 3.03 | 2.98 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 10 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 2628 | FC Znamya Noginsk vs Khimki M | 2.51 | 3.48 | 2.41 |
| 14:00 | 2830 | Prachuap FC vs Chonburi | 3.57 | 3.47 | 1.88 |
| 14:00 | 3285 | FC Tver vs FC Kairat Moscow | 1.42 | 4.90 | 6.40 |
| 14:00 | 4139 | Kolomna vs Peresvet Podolsk | 5.57 | 4.32 | 1.45 |
| 14:00 | 5988 | Nakhon Ratchasima vs Bangkok Glass | 5.59 | 3.57 | 1.56 |
| 14:30 | 1895 | Suphanburi vs Chiangrai Utd | 3.57 | 3.18 | 1.98 |
| 15:00 | 1173 | Indjija vs FK Loznica | 1.32 | 5.00 | 9.60 |
| 15:00 | 1972 | FK Zlatibor vs FK Imt Novi Beograd | 2.20 | 2.99 | 3.23 |
| 15:00 | 2423 | Leningradets vs Dinamo St Petersburg | 1.35 | 4.73 | 6.75 |
| 15:00 | 2482 | Baltika-Bfu Kaliningrad vs Zenit II SP | 2.55 | 3.17 | 2.55 |
| 15:00 | 3581 | FK Zarkovo vs FK Kabel Novi Sad | 1.32 | 5.00 | 9.60 |
| 15:00 | 4430 | Pattaya United FC vs Muang Thong Utd | 2.61 | 3.57 | 2.29 |
| 15:00 | 5986 | FC Olymp-Dolgoprudny vs 2-Znamya | 1.88 | 3.52 | 3.52 |
| 15:30 | 2339 | Berane vs OFK Titograd | 1.55 | 3.52 | 5.79 |
| 15:30 | 4110 | Komarno vs Zemplin Michalovce | 3.70 | 3.46 | 1.85 |
| 15:30 | 4537 | Grbalj vs Bokelj | 6.80 | 4.10 | 1.50 |
| 15:30 | 4798 | Jedinstvo BP vs Mladost DG | 1.54 | 4.00 | 6.20 |
| 15:30 | 5079 | Kom vs FK Arsenal Tivat | 5.37 | 3.41 | 1.61 |
| 15:30 | 5496 | FK Cetinje vs OFK Igalo 1929 | 6.00 | 3.75 | 1.59 |
| 15:45 | 4385 | Central Espanol FC vs Juventud LP | 2.50 | 3.17 | 2.60 |
| 16:00 | 5661 | Dinamo Briansk vs Zenit Penza | 1.22 | 5.59 | 9.63 |
| 17:00 | 3520 | Lokomotiv II M vs FC Murom Murom | 1.75 | 3.72 | 3.86 |
| 17:30 | 2799 | Al Khaleej Club vs Alshoulla | 2.50 | 3.35 | 2.75 |
| 17:45 | 4985 | AL Draih vs Al Jabalain | 3.81 | 3.47 | 1.82 |
| 18:00 | 3057 | FC Saransk vs Saturn Ramenskoye | 1.43 | 4.24 | 6.16 |
| 18:20 | 2999 | Jeddah Club vs Bisha FC | 2.06 | 3.28 | 3.23 |
| 19:00 | 1706 | Tijuana U20 vs Pachuca U20 | 2.75 | 3.19 | 2.37 |
| 19:00 | 1822 | Javor Ivanjica vs FC Rad | 1.55 | 3.85 | 6.40 |
| 19:00 | 3737 | Macva Sabac vs FK Zeleznicar Pancevo | 1.81 | 3.25 | 5.00 |
| 20:00 | 2247 | Leioa vs Guijuelo | 2.65 | 3.42 | 2.32 |
| 20:00 | 5339 | Kosovo vs Jordan | 1.94 | 3.55 | 3.80 |
| 21:00 | 1571 | Schweinfurt vs Buchbach | 1.79 | 3.71 | 3.66 |
| 21:00 | 1826 | Lokomotive Leipzig vs Energie Cottbus | 2.36 | 3.61 | 2.50 |
| 21:00 | 1882 | Kray vs Sportfreunde Baumberg | 2.65 | 4.04 | 2.11 |
| 21:00 | 1911 | SC Staaken 1919 vs SV Victoria Seelow | 1.26 | 5.79 | 7.33 |
| 21:00 | 3011 | SV Linx vs Reutlingen | 2.56 | 3.87 | 2.22 |
| 21:30 | 2003 | Sportfreunde Lotte vs Wiedenbruck | 4.24 | 3.52 | 1.72 |
| 21:30 | 4389 | Puerto Nuevo vs Central Ballester | 1.92 | 3.45 | 4.00 |
| 21:30 | 4522 | Yupanqui vs Csyd Liniers | 3.87 | 3.34 | 1.85 |
| 21:30 | 4564 | Sportivo Barracas vs Centro Espanol | 2.11 | 3.03 | 3.37 |
| 21:30 | 4863 | CA Lugano vs Argentino Rosario | 3.35 | 3.15 | 2.24 |
| 21:30 | 5487 | Telfs vs SV Fugen | 1.18 | 6.73 | 9.42 |
| 21:45 | 3735 | Skiljebo SK vs FC Arlanda | 1.01 | 13.47 | 38.47 |
| 22:00 | 1148 | Walsall vs Forest Green | 2.50 | 3.26 | 2.54 |
| 22:00 | 1289 | Wigan vs Shrewsbury | 1.69 | 3.58 | 4.35 |
| 22:00 | 2746 | Exeter vs Bristol Rovers | 1.99 | 3.42 | 3.28 |
| 22:30 | 2816 | Catania vs Vibonese Calcio | 1.70 | 3.56 | 4.95 |
| 22:30 | 4853 | Cordoba vs CD Ebro | 1.28 | 4.84 | 9.09 |
| 23:00 | 5437 | Lyon W vs Bayern Munich W | 1.61 | 3.87 | 4.55 |
| 23:00 | 5845 | SL Benfica W vs Kopparbergs Go W | 1.87 | 3.71 | 3.38 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatano Novemba 10, 2021

Nipashe



Pogba aondolewa kikosi cha Ufaransa

UKURASA 21

HESABU...



Mohamed Hussein 'Tshabalala' akipiga hesabu za kumtoka Kibu Denis katika mazoezi ya Taifa Stars, yaliyofanyika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana, kujiandaa na mchezo dhidi ya DR Congo kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia nchini Qatar mwakani. Nyuma ya Kibu ni Mbwana Samatta. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# FRANCO ATOA SABABU KUKUBALI KUTUA SIMBA

## Awataja mashabiki, Onyango akataa kwenda kuichezea Harambee Stars akimsubiri, Sakho na Kanoute...

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba wakieleza kurejea kwa wachezaji wao watatu waliokuwa majeruhi, Kocha Mkuu mpya wa timu hiyo, Mhispania Pablo Franco, ameeleza furaha yake ya kujiunga nao na kuanika sababu zilizomvutia kukubali kutua kukinoa kikosi hicho.

Simba juzi ilitangaza kuingia mkataba wa miaka miwili na Franco ambaye aliwahi kuwa Kocha Msaidizi wa Real Madrid mwaka 2018, lakini mwaka 2015 akiinoa Getafe kama kocha mkuu kwa kuiongoza kwenye Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga.

Hata hivyo, Franco ambaye ametua Simba akitokea Al-Qadsia ya Kuwait, hakuwahi kuzungumza chochote tangu akubali kuingia mkataba na Simba, lakini jana alitupia video fupi katika mtandao wa kijamii akieleza furaha yake ya kujiunga na mabingwa hao wa Tanzania Bara.

"Nimefurahi kujiunga na Simba, ni timu kubwa Afrika ina mashabiki wengi na ina matarajio makubwa jambo ambalo limenivutia. Simba Nguvu Moja," alisema Franco.

Hata hivyo, wakati mashabiki wa Simba wakifurahia kumpata kocha huyo wa daraja la juu kisoka, furaha hiyo itakuwa imeongezeka mara mbili zaidi baada ya habari njema ya kurejea kwa wachezaji wao watatu kati ya watano wa kikosi cha kwanza walikuwa majeruhi. Chumba cha majeruhi cha Simba, kilikuwa na wachezaji watano muhimu wa kikosi cha kwanza, lakini sasa wamebaki wawili baada ya klabu hiyo kutangaza kurejea mazoezini kwa viungo Sadio Kanoute, Pape Ousmane Sakho na Mzamiru Yassin.

"Sadio Kanoute, Pape Ousmane Sakho na Mzamiru Yassin, wamepona majeraha yao na wamerudi uwanjani wakiwa fiti kwa asilimia 100," ilieleza taarifa hiyo ya Simba.

Tayari Kanoute na Sakho wameanza mazoezi pamoja na wenzao tangu juzi wakati Mzamiru amejiunga na kikosi cha timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars kinachojiandaa na mchezo wa kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia dhidi ya DR Congo, mchezo utakaopigwa kesho katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Wachezaji wengine waliokuwa majeruhi, Kiungo Taddeo Lwangwa, uongozi wa Simba ulieleza yeye bado anauguza jeraha na amepewa mapumziko ya wiki mbili kabla ya kurejea uwanjani kuuwahi mchezo dhidi ya Ruvu Shooting utakakaopigwa Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza Novemba 19, mwaka huu.

Kuhusu mshambuliaji Chris Mugalu, "yeye ataendelea kukosekana kwa sababu ya jeraha linalomsumbua kutopona vizuri, hivyo amepewa muda ili awe fiti kwa asilimia 100".

Katika hatua nyingine, Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Kenya, 'Harambee Stars', Mturuki Engin Fırat, ameeleza changamoto anayoipitia baada ya kuwakosa mabeki wake watatu wa kati tegemeo aliowaita katika kikosi hicho kinachojiandaa na mechi ya kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia dhidi ya Uganda kesho, Alhamisi.

Fırat alisema katika mchezo huo atawakosa mabeki wa kati Joash Onyango wa Simba ambaye amekataa kujiunga na Harambee Stars baada ya kuamua kubaki na klabu yake.

"Nitawakosa Joseph Okumu [anayeichezea Gent ya Ubelgiji] ambaye ni majeruhi, pia Joash Onyango na Brian Mandela [Mamelodi Sundowns] wamegoma kujiunga na timu ya taifa baada ya kuamua kubaki ki na timu zao," alisema Fırat.

## Waziri Mkuu atoa neno Stars, Samatta...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Waziri Mkuu wa Tanzania, Kassim Majaliwa jana, akitembelea mazoezi ya Taifa Stars na kuwataka wachezaji kutowaangusha Watanzania, nahodha wa timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, Mbwana Samatta, amesema mechi yao dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, itakayochezwa kesho, Alhamisi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, ndiyo itakuwa muhimu zaidi kushinda kwa sababu itawaonyesha dira ya nini watakachotakiwa kufanya kwenye mchezo wa mwisho.

Akizungumza na wachezaji Uwanja wa Benjamin Mkapa katika mazoezi ya timu hiyo, Majaliwa alisema Watanzania wanaimani kubwa na Taifa Stars, na kuwataka kuhakikisha wanapata ushindi katika mchezo huo muhimu wa kesho na kisha dhidi ya Madagascar ugenini Jumapili.

Awali, Samatta baada ya kuwa mchezaji wa mwisho kujiunga kwenye kikosi hicho kinachojiandaa na mechi ya kusaka tiketi ya kufuzu fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika mwakani nchini Qatar, alisema japo wanakabiliwa na mechi mbili kabla ya kumaliza hatua ya makundi dhidi ya DR Congo na Madagascar, lakini mechi ya kesho dhidi ya Wakongomani hao ndiyo muhimu zaidi kushinda ili kujiweka kwenye mazingira mazuri zaidi.

"Tuko vizuri, nimefika nimekuta wachezaji wenzangu wapo kambini, tumejiandaa kupambana na tunawaomba mashabiki wetu watuunge mkono, kwa sababu tunakwenda kucheza mechi mbili za mwisho zitakazotoa mwelekeo, lakini hii ya Alhamisi ni muhimu zaidi kwetu na ni muhimu kushinda kwa sababu ndiyo itakayotoa mwanga wa nini kinatakiwa kufanyika kwenye mechi ya mwisho," alisema straika huyo anayeichezea Antwerp ya Ubelgiji kwa mkopo akitokea Fenerbahce ya Uturuki.

Baada ya mchezo huo wa kesho Taifa Stars itamalizia mechi yake ya Kundi J, Novemba 14 ugenini kwa kucheza dhidi ya Madagascar.

Stars inaliongoza Kundi J, ikiwa na pointi saba sawa na Benin, lakini ikiwa imefunga mabao matano na kufungwa manne, Benin ikifunga matatu na kufungwa mawili, wakati DR Congo yenyewe ikiwa na alama tano ikifuatiwa na Madagascar yenye pointi tatu mkiani. Kinara wa kundi, atakwenda kucheza mechi za mtoano na vinara wengine wa makundi A hadi I, kupata timu tano zitakazokwenda Qatar kuliwakilisha Bara la Afrika katika fainali hizo za dunia.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >